
# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 21 | Januari 22, 2022 NAKALA BILA MALIPO


# NDOTO YA UHC

**Hali ya kutoelewana katika NHIF imewanyima Wakenya huduma bora na nafuu za matibabu. Huku polisi na walimu wakihamia kwa kampuni za kibinafsi, mpango wa serikali unaelekea kuzama. Tunafichua migawanyiko mibaya katika shirika hilo na kuelezea ni kwa nini Huduma ya Afya kwa Wote imebakia kuwa ndoto.**

# *The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore*

# anywhere, anytime.

Follow the link to subscribe

> ***epaper.nation.africa.***

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play




Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111
Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION e ePaper

kauli ya mhariri

## Yaliyomo

**10 'HANDISHEKI' TULI YA RUTO-RAILA:** Waziri Mkuu wa zamani aliwatuma washirika wake wote waliochaguliwa kumkaribisha William Ruto wakati wa ziara yake ya juzi Nyanza, huku hatua ya Rais katika eneo hilo ikiacha wengi na maswali.

**15 JANGA LA MITANDAO YA KIJAMII:** Usiwape watoto wako simu za mkononi. Wamo hatarini kubwa ya kushawishiwa na matapeli kujaribu mambo hatari, na mwishowe, hali inakuwa wao kulazwa hospitalini.

**20 KWAKO IG, RAIA SI MAADUI WAKO:** Machoni mwa wananchi, maafisa wa polisi ni wanyang'anyaji wanaotumia sare zao na silaha kujinufaisha.

**25 'SHUKURU MUNGU UKO HAI!'** Simu zinaaza kulia tena, na kuleta fuhara lakini pia majonzi na hasira huku wakazi wa Tigray wakiweza kuwasiliana tena.



- *Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

# Lazima serikali izingatie UHC ili kutoa huduma za afya kwa Wakenya wote

Baadhi ya huduma muhimu serikali yoyote ile inaweza kutoa kwa raia wake ni usalama, afya na elimu. Haya ni majukumu nyeti na yenye mahitaji mengi na utawala wowote unaoyapuuza utachukuliwa kuwa serikali mbaya iliyojengwa kwenye msingi wa uongozi duni na hatari.

Hakika, uboreshaji wa idara hizi mara nyingi huangaziwa kwa maneno matupu kwenye kampeni. Utawala wa Kenya Kwanza uliahidi kuwa mengi yatafanywa kuboresha huduma za afya kwa mamilioni ya Wakenya wasioweza kuzigharamia.

Katika kampeni kali mwaka jana, Rais William Ruto aliomba kura kwa kuvumisha zaidi suala la afya kwa Wakenya wote. Raia walihakikishiwa kuwa baada ya kuingia afisini, serikali yake itaanzisha mpango wa Afya Kwa Wote (UHC), kuhakikisha Wakenya wote wanaenda hospitalini na kutibiwa bila malipo.

Mpango wa UHC unamaanisha hali ambapo watu binafsi na jamii hupata huduma bora za afya kwa gharama nafuu. Mpango wa kutoka huduma hii si jambo geni. Suala hilo limezungumziwa kwa muda mrefu lakini utekelezaji wake haujafaulu. Ahadi ya kuuwezesha kufaulu wakati huu bado inaonekana kuwa ndoto.

Asasi kuu iliyopangiwa kutekeleza mpango huo ni Hazina ya Bima ya Kitaifa ya Hospitali (NHIF). Wachangiaji wakuu wa hazina hii ni Wakenya waliojiriwa katika sekta rasmi, wanaolipa kwa kukatwa kwa mishahara yao kila mwezi. Kwa waajiriwa hawa, ni lazima kuchangia,



**Allan Buluku**

**Kikwazo kikuu katika utekelezaji wa UHC ni ufadhili usiotosha kutoka kwa serikali. Sekta ya afya hupokea asilimia sita pekee ya bajeti nzima. Ili mpango huu bora kuanza kunawiri, lazima serikali iongeze idadi ya Wakenya watakaohudumiwa na NHIF, ivutie watu wengi katika sekta isiyo rasmi walipe michango yao, na ihakikishe vituo vya afya vina dawa na wahudumu waliohitimu ili kuvutia Wakenya wengi katika hospitali za umma.**

ilhali walio katika sekta zisizo rasmi, ambao ni asilimia 83 ya idadi jumla ya wafanyakazi nchini, sio lazima.

Kwa hivyo, wachangiaji wakuu kwa hazina hii ni wachache kuliko wanaofaidi, na wengi wao ni watumishi wa umma, walimu na polisi. Hivi majuzi, Huduma ya Kitaifa ya Polisi iliondoa wanachama wake katika NHIF, ishara mbaya isiyovutia imani kwa asasi hiyo.

Kikwazo kikuu katika utekelezaji wa UHC ni ufadhili usiotosha kutoka kwa serikali.

Sekta ya afya hupokea asilimia sita pekee ya bajeti nzima. Ili mpango huu bora kuanza kunawiri, lazima serikali iongeze idadi ya Wakenya watakaohudumiwa na NHIF, ivutie watu wengi katika sekta isiyo rasmi walipe michango yao, na ihakikishe vituo vya afya vina dawa na wahudumu waliohitimu ili kuvutia Wakenya wengi katika hospitali za umma.

Wakati huu, hata walio na kadi za NHIF bado huchelea kwenda katika hospitali za umma; hujibebesha mzigo kwa kulipia huduma za afya katika hospitali za kibinafsi zinazotoza ada ghali. Katika nchi ambako mpango wa UHC umedumu kwa muda mrefu, watu wote - matajiri na maskini - hupata huduma katika hospitali zao za umma zilizo na vifaa vya kutosha.

Nchi hizo huepuka aibu ya viongozi kwenda nchi za kigeni kwa matibabu ilhali wangekuwa na huduma hizo nyumbani, kama wangejitolea kuhakikisha mifumo inafanya kazi.

UHC ni mpango mzuri unaoweza kuokoa maisha ya Wakenya wengi na unapasa kupewa uzito unaohitaji.

***abuluku@ke.nationmedia.com***

- *Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

Darubini ya Wiki
Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno
**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Joe Ageyo** Mkurugenzi wa Uhariri
**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji
**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

■ Masit achunguzwa kuhusu uchaguzi

# Jopokazi la IEBC larudi kwa vikao

Jopokazi lililobuniwa kuchunguza makamishna wanne wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) litaanza tena vikao vyake wiki hii baada ya likizo ndefu ya Desemba.

Jopokazi hilo, likiongozwa na Jaji Aggrey Muchelule Jumatatu litaendelea kusikiliza kesi dhidi ya kamishna aliyesimamishwa kazi Irene Masit katika Taasisi ya Kitaifa ya Kubuni Mtaala (KICD) jijini Nairobi.

Masit, mmoja kati wa makamishna wanne waliosimamishwa kazi na Rais William Ruto mwaka jana, anachunguzwa na jopokazi hilo kuhusu tabia yake katika uchaguzi wa urais wa Agosti 9. Pamoja na Juliana Cherera, Justus Nyang'aya na Francis Wanderi, walikataa matokeo ya urais yaliyotangazwa na aliyekuwa mwenyekiti wa IEBC Wafula Chebukati.

Hii ni baada ya Bunge kuidhinisha pendekezo lililomtaka Rais kubuni jopokazi la kuchunguza tabia yao. Makamishna wengine watatu walijiuzulu. Lakini Masit alisimama kidete na amepinga mchakato wa kumuondoa.

Jopokazi hilo lilianza vikao Desemba 20, 2022 na linatarajiwa kutoa ripoti kwa Rais Ruto baada ya kukamilisha uchunguzi ndipo amuzi utolewe kuhusu hatima ya Masit.



Irene Masit na Justus Nyang'aya katika mkahawa wa Pride Inn mnamo Septemba 17, 2022. PICHA | WACHIRA MWANGI

■ Verstappen atafuta taji lake la tatu mfululizo



Max Verstappen wa Red Bull akishiriki shindano la Japanese Grand Prix mjini Suzuka, Japan mnamo Oktoba 9, 2022.

# Msimu mrefu zaidi wa F1 wa mbio 23

Msimu wa Formula One utakuwa mrefu zaidi kuwahi kushuhudiwa huku ukiwa na mashindano 23 mwaka huu, waandalizi walisema Jumanne licha ya kushindwa kupata mwenyeji mpya wa shindano la The China Grand Prix.

Mafisa wakuu wa Formula One wamekuwa wakitafuta nchi ya kuchukua nafasi hiyo tangu walipotangaza mnamo Desemba kuhusu kufutiliwa mbali kwa Grand Prix ya China kwa mwaka wa nne mfululizo wakitaja matatizo yanayoendelea kuhusiana na janga la Covid-19.

Ureno na Uturuki zimekisiwa kujaza pengo hilo kwa sababu zote zina tajriba ya kuwa wenyeji wa Grand Prix. Formula 1 ilitoa taarifa Jumanne ikisema ratiba itabakia mashindano 23 na kuacha pengo kubwa kati ya shindano la tatu, Australian Grand Prix Aprili 2, na shi- Azerbaijan mnamo Aprili 30.

"Formula 1 inathibitisha msimu wa 2023 utajumuisha mashindano 23. Tarehe zote zilizowekwa za mbio hazijabadilika."

Max Verstappen wa Red Bull atazindua azma yake ya kuwania taji la dereva kwa mara ya tatu mfululizo katika taifa la Bahrain mnamo Machi 5.

■ Wanaunga mkono M23, asema Tshisekedi

# DRC: Rwanda kiini cha mapigano



Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo Felix Tshisekedi ameishutumu Rwanda kwa kuwa chanzo cha machafuko eneo hilo, akijibu madai ya waziri wa Rwanda, Claire Akamanzi, katika Kongamano la Kimataifa Kuhusu Uchumi, mjini Davos, Uswizi.

"Samahani madam, suala la ukosefu wa usalama linalotukabili eneo la Maziwa Makuu linaitwa Rwanda," akasema. Aliongeza kuwa "Rwanda inaunga mkono waasi wa M23" kutishia usalama mashariki mwa DRC – dai ambalo Rwanda imekanusha. Aliwalaumu waasi hao kwa kuua raia zaidi ya 100 katika eneo la Kishishe ili "kuwafurusha" kutoka kijiji hicho.

■ Kampuni imewekwa chini ya usimamizi

# Shirika la betri Uingereza yafungwa



Britishvolt, kampuni ya Uingereza inayohusika na mpango wa kutengeneza betri za umeme za magari, ilisambaratika Jumanne baada ya kukumbwa na changamoto za kifedha.

Kampuni hiyo chipukizi iliyopigiwa debe na aliyekuwa waziri mkuu Boris Johnson kupiga jeki juhudi za kupunguza uchafuzi wa anga, imekuwa ikiendesha mradi huo wa mabilioni ya pesa jijini Blyth, Kaskazini Mashariki mwa Uingereza.

Lakini Jumanne, iliingia mikononi mwa usimamizi, mchakato ambapo kampuni inayokabiliwa na matatizo huleta wataalam kutoka nje ili kujaribu kuokoa sehemu za biashara.

*- Zimetafsiriwa na Mary Wangari*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ UHUSIANO WA KARIBU WAIBUKA KATI YA MCK NA SERIKALI

# MATEKA: WANAHABARI WAYUMBA

Dennis Itumbi ni mmoja wa watu wenye ushawishi mkubwa katika mitandao ya propaganda ya Rais William Ruto. Anaongoza vita vya mtandaoni na hulenga sana mashirika makubwa ya habari na wanahabari wakuu anaodai hawampendi Rais.






Tulimpigia simu Mkuu wa Huduma ya Mawasiliano ya Rais David Mugonyi kwa ufafanuzi kuhusu majukumu halisi ya kazi katika serikali inayoonekana kuwapa watu tofauti majukumu yanayofanana, lakini hakupokea simu zetu wala kutupigia.

Kama uhusiano wa serikali ya Ruto na wanahabari unategemea orodha za maadui na marafiki inavyoashiriwa katika mitandao ya kijamii, basi Itumbi na wenzake wanashikilia nyadhifa zenye ushawishi mkubwa.

Ingawa anakaribisha mazungumzo kati ya wadau wa sekta ya habari na serikali, Mkuu wa Chama cha Wanahabari wa Kujitegemea Oloo Janak anataka mchakato ambapo mashirika yote yanayowakilishwa katika MCK yanatambuliwa.

Hali ya kushukiana, iliyoponza Kundi la Kufanyia Mabadiliko Sekta ya Habari Kenya, baada ya kujiondoa kwa Baraza la Wanahabari, imesababisha hali inayoweza kufaidi watu wanaotaka kutumia mbinu ya gawanya-utawale katika suala la uhusiano wa serikali na wanahabari.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Uchumi Dijitali, Eliud Owalo, amekuwa na msururu wa mikutano na wadau wa sekta ya habari siku za hivi majuzi. Je, sera ya wanahabari inaongozwa na kundi linalomzunguka Ruto katika Ikulu au ni warasimu katika wizara?

Waziri na Katibu wake Edward Kisiang'ani huenda wametambua migawanyiko ndani ya sekta hiyo ambayo inaweza kutatiza juhudi za kuwa na msimamo mmoja kuhusu masuala kama sheria inayosubiriwa, deni la matangazo ya serikali na hakikisho la uhuru wa wanahabari.

## Kama serikali ya Ruto itaweka sera zake kutaka kuteka vyombo vya habari kupitia presha ya uchumi, kushinikiza kufutwa kazi kwa wanahabari wanaoonekana kuipinga na kutumia washirika wake kudhibiti Baraza la Vyombo vya Habari, basi huenda hali itakuwa ngumu

● Na MACHARIA GAITHO

Wakati aliyekuwa Mhariri Mkuu wa Nation Media Group Mutuma Mathiu katika makala yake ya kila wiki hivi majuzi alipozua ugomvi na mtetezi wa Rais William Ruto katika mitandao ya kijamii Dennis Itumbi, huenda ilionekana kuwa ujinga wa kualika nguruwe katika shindano la kupigana mieleka ndani ya matope.

Itumbi alirukia nafasi hiyo kujadiliana katika jukwaa ambapo inaweza kusemekana ni mmoja wa watu wenye ushawishi Kenya, akiheshimiwa kwa kuwa na wafuasi wengi wa mtandaoni ambao huwa tayari kushiriki vita katika Twitter.

Ilhali, zaidi ya ugomvi kati ya watu wawili hao ambao ni wazi wanachukiana, kulikuwa na masuala ambayo yanaweza kuelezea uhusiano wa Rais Ruto na wanahabari.

Ingawa hana wadhifa rasmi, na hata katika orodha ya walioteuliwa majuzi kwa nyadhifa kuu za Huduma ya Mawasiliano ya Rais hakuwepo, Itumbi anatambuliwa sana kuwa mmoja wa watu wenye ushawishi katika mawasiliano ya Ruto na mitandao ya propaganda.

Ndiye huelekeza vita vya mtandaoni kwa niaba ya Ruto, na anapenda kulenga mashirika makubwa ya habari na wanahabari maarufu anaodai hawampendi Rais.

Kabla ya uchaguzi mkuu wa Agosti 2022, Itumbi na wanachama wengine wa mawasiliano wa Ruto waliongoza vita katika mitandao ya kijamii dhidi ya wanahabari waliodai hawakupenda Ruto.

Mnamo Novemba Mutuma alipoondoka kama Mkuu wa Uhariri wa NMG, Itumbi na wenzake walisherehekea katika mitandao ya kijamii. Kuondoka kwa Mutuma kulitokea wakati mmoja na kubadilishwa kwa Mhariri Msimamizi wa Daily Nation Bernard Mwinzi aliyepunguziwa majukumu katika kampuni hiyo.

Kisha kulifuatia kuachishwa kazi kwa

Endelea Uk 6

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Serikali inanuia kushika mateka wanahabari?

Kutoka Uk 5

mwanahabari Vincent Achuka, na furaha ya Itumbi na kundi lake ilionyesha kwamba waliokuwa katika orodha yao ya lawama walikuwa njiani kuondoka.

Kama uhusiano wa serikali ya Ruto na wanahabari unategemea orodha za maadui na marafiki inavyoashiriwa katika mitandao ya kijamii, inaonekana wazi kuwa Itumbi na wenzake wanashikilia nyadhifa zenye ushawishi kwa kuzingatia utangamano wao na wanahabari siku baada ya siku.

Hiyo ndiyo sababu, huku Waziri wa Habari, Mawasiliano na Uchumi Dijitali, Eliud Owalo, na Katibu wake, Edward Kisiang'ani, wakifanya misururu ya mikutano na wadau katika sekta ya habari majuzi, macho hayaelekezwi kwa matokeo ya majadiliano hayo, lakini iwapo uwezo kamili wa sera ya habari uko kwa kundi linalomzunguka Ruto katika Ikulu badala ya kuwa na warasimu katika Wizara.

Labda mfano mmoja utatosha. Katika miaka ya mwanzo ya utawala wa Jubilee ya Rais Uhuru Kenyatta na naibu wake Ruto, aliyekuwa Katibu wa Habari, Joseph Tiampati, aliita mkutano wa wanahabari wakuu kuchangia maoni kuhusu stakabadhi iliyotayarishwa kuongoza kuundwa kwa sera za mawasiliano ya serikali na miundo yake. Katikati ya majadiliano katika ukumbi wa mikutano, Itumbi na wenzake waliingia kwa kishindo na kutangaza kwamba walitoka Ikulu.

Tiampati aliwaeleza kilichokuwa kikifanyika, lakini hawakufurahia na wakatangaza wazi kuwa mpango huo wote ulikuwa wa kuharibu wakati kwa kuwa Rais alikuwa msemaji wake mwenyewe na hakuhitaji usaidizi kutoka yeyote. Huo ndio ulikuwa mwisho huku Tiampati akishindwa na kunyenyekea kwa mamlaka aliyoonyeshwa na wadogo wake katika serikali na akafunga mkutano.

Itumbi na wenzake wakati huo walikuwa wakihudumia Rais Kenyatta kabla ya kutimuliwa Ikulu kwa kuhamishia uaminifu wao kwa naibu wake Ruto, aliyekuwa ametofautiana na mkubwa wake wakati huo.

Sasa wamerudi katika nyadhifa kubwa katika Ikulu ya Ruto, na kama tabia waliyoonyesha wakati wa kampeni ndiyo mwongozo, basi ndio wanaosikilizwa na Rais kuhusu jinsi ya kuhusiana na wanahabari.

Hivi vinaweza kuwa aina ya vizingiti vya ndani ambavyo Owalo na Kisiang'ani watalazimika kuhimili wanapokutana na makundi tofauti ya wadau wakiahidi serikali itaunga mkono uhuru wa wanahabari lakini katika mazingira ambayo sera inaweza kuamuliwa na vigezo vya nje kama vile ni nani anayeaminika na watu muhimu wanaomzunguka Ruto na ni nani anayeshukiwa.

Hayo yakijiri, Waziri na Katibu huenda wametambua migawanyiko ndani ya sekta hiyo ambayo inaweza kutatiza juhudi za kuwa



Wapiga picha za televisheni katika Mahakama Kuu ya Mombasa. Kampuni nyingi za kutoa matangazo zinahamia kwa majukwaa ya kidigitali . PICHA I KEVIN ODIT

na msimamo mmoja kuhusu masuala kama sharia inayosubiriwa, deni la matangazo ya serikali, hakikisho la uhuru wa wanahabari, na pengo katika Baraza la Wanahabari Kenya kufuatia kukamilika kwa muhula wa wanachama wake.

Hali ya wadau kushukiana, iliyodhoofisha Kundi la Kufanyia Mabadiliko Sekta ya Habari Kenya, baada ya kujiondoa kwa Baraza la Wanahabari, imesababisha hali inayoweza kufaidi watu wanaotaka kutumia mbinu ya gawanya-utawale, katika suala la uhusiano kati ya serikali na wanahabari. Kufikia wakati wa kuandika, maafisa wakuu wa serikali walikuwa wakizungumza na Baraza la Wanahabari pekee, ambalo kwa wakati huu linasimamiwa na Afisa Mkuu Mtendaji David Omwoyo kwa kuwa hakuna baraza.

Hata hivyo, Rais wa Chama cha Wahariri Churchill Otieno na Katibu Mkuu wa Chama cha Wanahabari Eric Oduor walithibitishia Darubini ya Wiki kuwa mashirika yao yamepanga mikutano na wanasubiri kuthibitisha tarehe za kukutana.

Kisichoeleweka ni iwapo kundi lote la wadau wa habari linaloleta pamoja Baraza la Wanahabari na makundi mengine kama Chama cha Wanahabari wa Kujitegemea Kenya, Chama cha Wanawake katika Habari Kenya, Watangazaji wa Dijitali Kenya, Vyombo vya Habari vya Kijamii Kenya, Chama cha Wanahabari wa Siasa, Chama cha Wataaalamu wa Utangazaji na Wamiliki wa Vyombo vya Habari watawasilisha malalamishi yao.

Jinsi ilivyo, baadhi ya makundi ya uwakilishi hayafurahii kinachoonekana kuwa uhusiano wa karibu unaoibuka kati ya Baraza la Wanahabari na serikali, kama kilichofanyika wakati wa utawala wa Uhuru, viongozi wa baraza hilo walipochukuliwa kuwa watiifu kwa Waziri Joe Mucheru.

Kulingana na Mkuu wa Chama cha Wanahabari wa Kujitegemea Oloo Janak, mbinu inayotumiwa na Baraza la Wanahabari inazua wasiwasi kwa sababu ni sawa na ambayo tangu 2019 ililipunguza kuwa sehemu ya wizara, likishinikiza sheria za kukadamiza wanahabari. Ingawa anakaribisha mazungumzo na serikali, Janak anataka mchakato ambao wadau wote wanaounda Baraza la Wanahari watambuliwa.

Hofu yake ni kuwa kama hakutakuwa na mashauriano ya wazi, kuna hatari ya mchakato wa kujaza nafasi zilizo wazi katika Baraza la Wanahabari kutokuwa wa haki, hasa kama afisi ya MCK na wizara zitaungana kushawishi kuwepo kwa kundi tiifu kwa Kenya Kwanza.

Anahimiza serikali isikilize wadau wote katika sekta ya habari na sio MCK pekee, akisema kwamba shirika hilo la kudhibiti sekta ya habari linafaa kuwa huru na kuwajibika kwa wadau na sio kwa serikali.

Analalamika kuwa taarifa zinazotolewa na MCK kufuatia mikutano na Owalo na Kisiang'ani zilitoa ishara mbaya kwa kuwa zinaashiria kwamba serikali, badala ya shirika huru - ndiyo inadhamini uhuru wa wanahabari.

Anasema kuwa ingawa inaweza kuombwa kutekeleza jukumu la kuwezesha, haiwezi kuongoza mchakato wowote wa kubadili-

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

sha sheria za habari au kujaza nafasi zilizo wazi katika Baraza la Wanahabari. Oduor, katika mazungumzo tofauti na Darubini ya Wiki, alikubaliana naye. Alifichua kuwa chama hicho cha wanahabari kimewasiliana na Owalo, lakini waziri alitaka kukutana kwanza na taasisi rasmi kama MCK kabla ya kukutana na wadau katika sekta hiyo.

Hata hivyo, ana hofu, kuhusu ripoti kutoka mikutano na Baraza la Wanahabari kwamba serikali inategemewa kutatua masuala yanayoathiri habari, akisisitiza kuwa suluhisho linatoka ndani ya sekta hiyo.

Mojawapo la masuala ambayo Baraza la Wanahabari lilifanya na wawakilishi wa serikali ni kukashifu wamiliki wa vyombo vya habari kwa kufuta wafanyakazi, pande zote mbili zikiashiria kuwa wawekezaji na mameneja wanaendelea kuwa matajiri huku wakihangaisha na kufuta kazi wanahabari.

Kisiang'ani, katika mkutano mmoja, alisema kuwa nyingi za Sh1.4 bilioni ambazo mashirika ya habari yanadai Shirika la Matangazo la Serikali, zimelipwa, na kuacha salio ya chini ya Sh250 milioni, lakini wanahabari wanaendelea kufutwa kazi. Oduor anakubaliana na wizara na MCK, akilaumu wamiliki wa vyombo vya habari kwa kutesa wanahabari, lakini anasema kupungua kwa mapato kunasababishwa na masuala tofauti zaidi ya deni la serikali. Anatoa mfano wa mabadiliko ya tekinolojia na watangazaji wakubwa kutumia mitandao ya dijitali na kuacha vyombo vya kawaida vya habari.



Rais wa Baraza la Wahariri Kenya Churchill Otieno

Serikali haiwezi kuelekeza biashara ya vyombo vya habari, lakini Oduor anatoa mfano wa Muungano wa Ulaya na mataifa mengine ambapo kampuni kubwa za dijitali kama Google, Facebook, YouTube na zingine zinalazimishwa na sheria, kutoa fidia kwa vyombo vya habari vya kawaida zinakotoa matini na kugawana matangazo. Msaada wa serikali kwa mipango kama hiyo katika sheria za habari Kenya unaweza kuzuia hali ya pesa kupotea. Anatarajia kuwa baada ya kukutana na mashirika kila moja kivyake, hatimaye Waziri atakutana na wadau wote pamoja.

Hata hivyo, hilo litategemea kumaliza migawanyiko iliyopo kwa wakati huu, ili Baraza la Wanahari liweze kurudi katika Kundi la Kufanya Mabadiliko katika Sekta ya Habari Kenya. Suala lingine ambalo litakuwa muhimu ni mtazamo wa Ikulu kwa wanahabari.

Serikali ya Ruto imeunda timu ya mawasiliano yenye nguvu ikiongozwa na mkuu wake wa miaka mingi wa habari David Mugonyi akiwa Mkuu wa Huduma ya Mawasiliano ya Rais. Aliyekuwa Msomaji Habari wa Citizen TV Hussein Mohamed aliteuliwa Msemaji wa Ikulu, huku Emmanuel Talam akiteuliwa Mkurugenzi wa Mawasiliano.

Wengine waliorudi baada ya kutimuliwa na Uhuru ni Munyori Buku kuwa Katibu wa Mawasiliano ya Umma; Eric Ng'eno, Mwandishi wa Hotuba na Mkurugenzi wa Kutoa Habari; James Kinyua, Mkurugenzi wa Chapa na Hafla; na David Nzioka kuwa Katibu wa Dijitali na Ubunifu. Aliyekuwa mwanahabari wa Nation na baadaye Mkurugenzi wa Mawasiliano wa chama cha United Democratic Alliance Wanjohi Githae aliteuliwa Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Umma.

Darubini ya Wiki ilimpigia simu Mugonyi kwa ufafanuzi kuhusu majukumu halisi ya kazi katika serikali inayoonekana kutoa nafasi ya kupatia watu tofauti majukumu yanayofanana, ikiwa na majenerali wanaozidi wanajeshi, lakini hakupokea au kujibu simu.



Wanahabari wa Nakuru wakilalamika kuhusu kunyanyaswa na polisi mnamo Januari 29, 2020.

Swali kubwa, hata hivyo, ni kuhusu kiwango cha ushawishi ambao timu hiyo ya mawasiliano itakuwa nao kwa sera ya habari.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*



Katibu Mkuu wa KUJ Eric Oduor

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ RUTO AMESHINIKIZA MARA KADHAA KUPANULIWA KWA MPANGO HUO NCHINI




Waziri wa Afya Susan Nakhumicha (kushoto) akipokea ripoti ya shughuli kutoka kwa Afisa Mkuu Mtendaji wa Mamlaka ya Kusambaza Dawa Kenya (Kemsa) Terry Ramadhani (kulia) wakati wa ziara katika maghala ya tawi la Kemsa eneo la Embakasi mnamo Novemba 8, 2022.

# VIKOSI VYA ULINZI VYAHEPA NHIF

## Lakini kuna hofu kuwa kwa kuwekewa bima na kampuni ya kibinafsi, polisi na maafisa wa magereza wanaweza kutumbukia mikononi mwa makundi yanayoweza kuwafanya mateka

● NA OSCAR OBONYO

Usajili wa kidijitali wa maafisa wa polisi na magereza ambao wamehama kutoka Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Hospitali (NHIF) hadi kwa bima mpya ya matibabu ya muungano wa CIC General umeanza, na kuzua maswali kuhusu uwezo wa serikali wa kufanya biashara nzuri na yenye faida na mashirika yake yenyewe.

Katika kinachoonekana kuwa bao la kujifunga, mashirika hayo mawili ya serikali - NHIF na Tume ya Kitaifa ya Huduma ya Polisi (NPSC) – yalisitisha mpango unaoendelea wa matibabu, na kutoa fursa kwa kampuni ya kibinafsi, CIC General Consortium, kutekeleza mpango huo.

Kwa njia fulani, hatua hiyo inatoa taswira tofauti ya uamuzi uliofikiwa na serikali miezi minne pekee kukuza umoja na ushirikiano wa kibiashara baina ya mashirika yake.

Huduma ya Afya kwa Wote (UHC) bado ni mojawapo ya miradi mikuu ya Rais William Ruto sasa na awali chini ya serikali ya Jubilee, aliyohudumia kama Naibu Rais. Rais ametoa wito mara kwa mara mpango huo upanuliwa kote nchini. Hata hivyo, mchakato wa kushughulikia zabuni husika Nambari: MICING/NPS/002/2022-2023 kwa ajili ya kutoa bima ya matibabu kwa polisi kupitia Idara ya Kitaifa ya Polisi (NPS) na maafisa wa magereza kupitia Idara ya Magereza Kenya (KPS), haujawa rahisi kama ilivyotarajiwa na wengi.

Zabuni hiyo, iliyotangazwa na NPS Desemba 7, 2022 na kufunguliwa Desemba 15, imepokea malalamishi na ukosoaji kutoka kwa baadhi ya wanasiasa, wafanyabiashara na maafisa wa serikali.

Akisema kuwa polisi wanatarajiwa kutoa huduma kwa wote, Mbunge wa Gatundu Kusini, Gabriel Kagombe, kwa mfano, anasema

Endelea Uk 8

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## kurunzi ya kenya

hatua ya serikali kuhamishia huduma muhimu za matibabu kwa makampuni ya kibinafsi ni jambo hatari ambalo litahatarisha huduma muhimu za polisi kwa Wakenya.

Akihojiwa majuzi, Mbunge huyo alidai hatua hiyo itavuruga mpango wa serikali wa kutoa huduma za afya kwa wote nchini. Mwanasiasa huyo anahofia hatua hiyo itaweka polisi na maafisa wa magereza mikononi mwa makundi "yatakayowageuza mateka."

Licha ya hofu hizo, jumla ya maafisa 141,961 ambao wanalengwa katika mpango wa matibabu - 109,557 kutoka NPS na 32,404 kutoka KPS – wanaonekana kuridhishwa na hatua hiyo mpya. Chini ya mpango huo na NHIF, maafisa 1,500 pekee - wengi wao wakiwa wa ngazi za juu - waliweza kupata huduma bora za afya.


Alipoulizwa maoni yake, msemaji wa NPS Dk Resila Onyango alisema uamuzi huo ulishinikizwa na masuala ya kifedha: "Tulihamia kwa Consortium kwa sababu walitoa zabuni ya chini zaidi na ya bei nafuu" akaeleza.

NHIF iliwasilisha ombi la kupewa upya kandarasi ya 2023 yenye thamani ya Sh9.3 bilioni, lakini ikashindwa na kundi la mashirika ya kibinafsi ya bima ya afya, CIC General Limited Insurance, Old Mutual General Insurance Kenya Limited na Britam General Insurance kwa gharama ya Sh8.6 bilioni.

Inasemekana kushindwa kwake kupata zabuni hiyo kulichangiwa na ulegevu na mivutano baina ya viongozi wake, pamoja na majaribio ya baadhi ya watu wa ndani kuongeza malipo. Zaidi, bima ya matibabu ilikuwepo wakati nafasi kadha za wasimamizi wa ngazi za juu, zikiwemo za wakurugenzi, zilikuwa wazi, hivyo kuathiri vibaya utoaji wa huduma. Uamuzi wa kusitisha zabuni ya NHIF pia ulijiri wakati Mwenyekiti wa bodi hiyo, Lewis Nguyai, na Afisa Mkuu Mtendaji Dkt Peter Kamunyo walikuwa wakizozana kuhusu usimamizi. Rais Ruto alimuondoa Nguyai, aliyekuwa Mbunge wa Kikuyu na kumteua Michael Kamau, aliyekuwa Waziri wa Uchukuzi.

Matatizo ya mpango wa matibabu wa NHIF-NPS yamekuwa yakiendelea kwa muda mrefu na, kwa mujibu wa duru za kuaminika, mashirika hayo mawili ya serikali yalifanya mikutano zaidi ya 20, nusu ya mikutano ikiwa katika ngazi ya usimamizi, huku iliyobaki ikihudhuriwa na viongozi wa ngazi za juu wa serikali kutoka idara husika, akiwemo aliyekuwa Katibu wa Usalama wa Ndani Karanja Kibicho na aliyekuwa Inspekta-Jenerali wa Polisi Hillary Mutyambai. Makampuni makubwa yalikuja tu kufuatia msururu wa malalamishi kuhusu utoaji wa huduma duni. Maafisa hao hawakufurahia walichoona kuwa huduma duni za hospitali kupitia NHIF. Awali, bodi hiyo ililalamika kuwa Sh4.5 bilioni zilizotengewa bima hazikutosha, jambo lililoilazimisha NPS kuongeza Sh200 milioni zaidi kwa mwaka ili kushughulikia madai hayo.

**Inasemekana kushindwa kwake kupata zabuni hiyo kulichangiwa na ulegevu na mivutano baina ya viongozi wake, pamoja na majaribio ya baadhi ya watu wa ndani kuongeza malipo. Zaidi, bima ya matibabu ilikuwepo wakati nafasi kadha za wasimamizi wa ngazi za juu, zikiwemo za wakurugenzi, zilikuwa wazi, hivyo kuathiri vibaya utoaji wa huduma. Uamuzi wa kusitisha zabuni ya NHIF pia ulijiri wakati Mwenyekiti na Afisa Mkuu Mtendaji wake walikuwa wakizozania uongozi**



Huduma ya Afya kwa Wote (UHC) ni mmoja wa miradi mikuu ya Rais William Ruto sasa na awali chini ya serikali ya Jubilee, ambayo alihudumia kama Naibu Rais.

Hata wakati huo, takwimu hazikuonekana kulingana na kilichotarajiwa kutoka kwa polisi - kuchunguza na kutaka uwajibikaji kuhusu matumizi ya pesa. Inasemekana NHIF haikutoa hesabu zilizokaguliwa za uchunguzi wala kujibu hoja za ukaguzi kutoka kwa mteja.

Kutokana na tofauti zisizoweza kusuluhika, NPS iliamua kutoa zabuni tena na kualika NHIF kuomba zabuni kama wahusika wengine wowote. Mwelekeo huo ulichochea vita baridi vilivyokuwepo baina ya mashirika hayo mawili ya serikali. NHIF iliripotiwa kupunguza huduma zake muda mfupi baadaye na kuwanyima huduma za afya maafisa zaidi ya 141,461 wa polisi na magereza.

Watu wa ndani wanadai NHIF pia ililemaza mifumo yake na kuwanyima huduma wote, isipokuwa maafisa wa ngazi za juu wapatao 1,500. Afisa mmoja wa ngazi za juu katika hazina hiyo alimwambia mwandishi huyu kuwa ni maafisa 39 pekee wa magereza wa ngazi za juu wanaoweza kupata matibabu maalumu, ambao ni wa viwango vya kazi N(14), P(6), R(14), S(4) na T(1), huku polisi 1,429 pekee kutoka viwango vya kazi M(455), N(607), P(247), R(97), na S(23) wakiweweza kupata huduma hiyo maalumu ya matibabu.

Hatua hii ilifungia nje idadi kubwa ya polisi chini ya bima ya matibabu ya NHIF ya KSh4.7 bilioni, jambo lililosababisha maelfu ya malalamishi kutoka kwa polisi wa ngazi za chini na watu wa familia zao.

Ni wakati huo ambao Kibicho na Mutyambai waliingilia kati na suala hilo likapelekwa kwa Baraza la Mawaziri. Uamuzi ulifikiwa wa kutafuta huduma mbadala za bima huku NHIF ikiendelea kulainisha shughuli zake.

Isipokuwa kuondoka kwa Nguyai kama mwenyekiti, haijabainika juhudi ambazo shirika hilo linachukua "kulainisha shughuli zake". Wakati huo huo, Kamau ameteuliwa na anatarajiwa kurekebisha mambo.

Kwa wakati huu, mgogoro kuhusu mchakato wa utoaji zabuni unaendelea, na pengine

hapa ndipo Kamau na Kamunyo wanafaa kuanzia juhudi zao za kulainisha mambo. Katika moja ya kesi hizo, ambayo Darubini ya Wiki imeona stakabadhi zake, Benedict Kabugi Ndungu wa Nairobi anamlalamika kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti Zabuni za Umma kwa anachokitaja kuwa "ukiukaji wa sheria katika zabuni ya kutoa bima ya matibabu kwa wanachama wa Idara ya Kitaifa ya Polisi na Idara ya Magereza Kenya".

Suala la mashirika kadhaa ya huduma za bima, anasema, linachanganya na si sahihi: "Hakuna kitu kinachoitwa muungano kama mzabuni anayestahili kutoa huduma za bima bali ni makampuni binafsi, mashirika ya serikali au ushirika. Fomu zote za kiwango cha kawaida za lazima katika Hati hii ya Kawaida ya Zabuni Mo.9 zinapaswa kujazwa na makampuni ya kibinafsi au makampuni ya serikali au ushirika. Hakuna fomu za kiwango cha kawaida za kundi la makampuni."


***oscar.tko@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ ZIARA YA RAIS ENEO HILO IMEACHA WENGI NA MASWALI



# "HANDISHEKI" TULI YA RUTO-RAILA

## Waziri Mkuu wa zamani, akiibuka mzoefu wa kujadiliana akiwa nje, alituma viongozi wake wote waliochaguliwa kumpokea Rais alipozuru Nyanza

• Na JOHN KAMAU

Baada ya Rais William Ruto kukamilisha ziara yake ya Nyanza, ambako alikaribishwa kwa mikono mwili na viongozi waliochaguliwa kutoka eneo hilo, swali moja ambalo halikujibiwa ni maana hasa ya uchangamfu ulioshuhudiwa.

Wakati wa ziara hiyo, Rais Ruto alikuwa mchangamfu. Alifanya mzaha kuhusu asilimia moja ya kura alizopata kutoka eneo hilo - na kuonekana kuashiria kuwa hilo ni suala ambalo sasa limepita. Vichekesho, furaha na urafiki vilionekana kuyeyusha uhasama.

Aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga, anayeendelea kuwa na uzoefu mkubwa wa kujadiliana akiwa nje, alikuwa ametuma viongozi wote waliochaguliwa kumlaki Rais. Ndugu yake, Oburu, alikuwepo pia. Ajenda ilionekana wazi na iliyopangwa. Orodha ya wazungumzaji ilionekana kupangwa kimakusudi. Mashambulio ya kawaida dhidi ya Waziri Mkuu wa zamani hayakuwepo - na waliohutubu walifanya hivyo kwa heshima.

Mtu anaweza kukisia tu kile Ruto hufanya kwa moyo wa nia njema. Kile wanachotaka wanasiasa wa Nyanza pia kinaweza kukisiwa tu. Ingawa Rais amesema hataki kuua upinzani, ushirikiano wao katika masuala yanayohitaji thuluthi mbili za kura bungeni ni muhimu. Jaribio la Ruto la kutafuta kuungwa mkono Nyanza ni la busara. Anajua wanasiasa wengi wa eneo hilo kwani alikuwa mwanachama wa ODM. Nao wanasiasa wa Nyanza wanaelewa madhara ya kutengwa kisiasa.

Kwa miaka mitano iliyopita, licha ya kuwa katika upinzani, eneo hilo lilipata nafasi katika serikali ya Uhuru Kenyatta kutokana na 'handisheki' kati ya Odinga na Rais Kenyatta. Kutokana na hilo, waliweza kufaidi kwa miradi mbalimbali na walipendelewa huku Rais Kenaytta akimtenga naibu wake, Dkt Ruto, na kuamua kufanyakazi na Odinga. Kuvunjika kwa uhusiano kati ya Jaramogi Oginga Odinga na Jomo Kenyatta mnamo 1966 kulichangia kutengwa kwa jamii ya Waluo. Isitoshe, eneo hilo lilinyimwa miradi ya serikali na hilo likawa funzo kubwa katika historia.

Kuundwa kwa chama cha Kenya Peoples Union kuliondoa Luo Nyanza serikalini. Viongozi wake hawangeweza kusafiri ng'ambo baada ya kunyimwa paspoti. Kutokana na kukata tamaa, alivyondika Bruce Mackenzie ba-

Endelea Uk 11

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

adaye 1968 kwa wanadiplomasia wa Uingereza, Jaramogi alikuwa amemwandikia Kenyatta barua kadhaa akiashiria kuwa alitaka kuridhiana na Kanu. Lakini, kulingana Mackenzie, "Mboya alisisitiza kuwa Odinga angemfikia kwanza badala ya Rais. Matokeo ni kwamba maelewano hayakufikiwa." Msimamo huo ulithibitishwa na Moi mnamo Novemba 1968 aliposema Odinga alipaswa kurudi Kanu bila masharti na "kumeza sera ya Kanu jinsi ilivyo leo."

Kifo cha Tom Mboya mnamo Julai 5, 1969 kilibadili hali ya kisiasa na Kenyatta akageuzwa kuwa mtu aliyechukiwa katika eneo la Nyanza. Zaidi, ni wachache ndani ya Kanu walithubutu kuhudhuria mazishi katika kisiwa cha Rusinga. Lakini miezi minne baadaye, Jomo Kenyatta alizuru Kisumu kufungua Hospitali ya Kuu ya Nyanza. Ziara hiyo ilibadili kabisa uhusiano kati yake na Jaramogi baada ya msafara wa magari yake kushambuliwa kwa mawe na kuzomewa kwa kelele za "Dume! Dume!"- kaulimbiu ya KPU.

Kufuatia ghasia hizo hadi kifo chake 1978, Kenyatta hakuwahi kukutana na Odinga wala kurudi eneo hilo. Zaidi, aliamuru kukamatwa na kuzuiliwa kwa viongozi wakuu wa KPU. Kenyatta hakutumia tu kisa cha Kisumu kama sababu ya kupiga marufuku KPU lakini hilo baadaye lilitumiwa na Rais Moi kumzuia Jaramogi kushiriki siasa za kitaifa.

Baada ya Odinga kuachiliwa Aprili 2, 1971, alijiunga tena na Kanu Septemba 8, 1971 na akaanza safari mpya ya kisiasa. Wakati huo, hasidi wake mkuu wa kisiasa, Tom Mboya alikuwa amekufa lakini alikuwa na kibarua cha kupambana na wanasiasa kama Odongo Omamo, Mathews Ogutu na Isaac Omolo Okelo, waliokuwa wamejaza pengo liloacha.

Jaribio la Odinga kuwania ubunge 1974 lilizimwa na Kanu baada ya baraza kuu la chama hicho kuamua kwamba ni wanachama wa KPU waliokuwa wanachama wa Kanu kwa miaka mitatu baada ya kutoka kizuizini ambao wangeidhinishwa kuwania. Watu hao pia walitakiwa wawe na "ufahamu kamili wa sera za serikali na chama na mipango ya maendeleo." Huo ulikuwa mwisho wa barabara kwa Odinga. Ingawa alichaguliwa mwenyekiti wa Kanu katika Wilaya ya Siaya mnamo 1975 na tena 1976, msajili wa chama hicho alikataa kuidhinisha kuchaguliwa kwake. Mnamo Aprili 1978, chama cha Luo Union kilituma ujumbe mkubwa kutafuta maridhiano na Kenyatta. Sasa inadaiwa hatua hiyo ilibatilishwa na Mkuu wa Mkoa wa Nyanza Isaiah Cheluget na viongozi waaminifu kutoka jamii ya Waluo na Wagusii - na ndiyo ilichochea ghasia mjini Nakuru.



Rais William Ruto akitaniana na Gavana wa Homa Bay Gladys Wanga ana viongozi wengine wa eneo hilo alipozindua Soko la Homa Bay mnamo Januari 13. PICHA I TONNY OMONDI

Baada ya Kenyatta kufa, Moi alitarajia kuvutia eneo hilo katika serikali yake. Alianza kurekebisha uhusiano na Jaramogi kwa kumteua mwenyekiti wa Bodi ya Pamba na Uuzaji Mbegu mnamo 1979. Ulikuwa wadhifa wa kwanza wa serikali kwa Jaramogi tangu 1966. Moi pia aliteuwa washirika Jaramogi - Luke Obok na Achieng Oneko - katika nyadhifa za mashirika ya serikali. Rafiki mwingine wa Odinga, Oloo Aringo aliteuliwa waziri mnamo 1980.

Hatimaye Julai 1980, Odinga alirudishwa Kanu kama mwanachama wa maisha na kuandaliwa kuingia bungeni baada ya kujiuzulu kwa Mbunge wa Bondo mnamo Machi 1981. Lakini alipodai, akiwa Mombasa mnamo Aprili 1984, kuwa Kenyatta alikuwa "mnyakuzi wa ardhi" Bw Odinga alizuiwa tena kuwania. Alibaki kwenye baridi ya kisiasa na kuanza kupigania mabadiliko akiwa nje ya serikali. Kuundwa kwa vuguvugu la Forum for Restoration of Democracy 1990 na kugawanyika kwake, baadaye, kulimnyima Odinga nafasi ya kuwa rais baada ya kuibuka wa nne nyuma ya Moi, Kenneth Matiba na Mwai Kibaki katika uchaguzi mkuu wa 1992.

Kutokana na kukata tamaa au labda hatua ya kimkakati, Odinga aliamua kufanya kazi na Kanu na akachukuliwa na Moi kuona miradi ya serikali katika Bwawa la Turkwel. Hatua hiyo ilisababisha uhasama ndani ya Ford Kenya na kuchangia kugawanyika kwake. Shida kuu ilikuwa uhusiano kati ya Odinga na Kanu.

Mnamo Mei 1993, Odinga alianzisha mpango wa kushirikiana na Kanu ili kusaidia kuleta maendeleo Nyanza. Alisema aliamini "kutokana na tajiriba chungu" kwamba, katika taifa la vyama vingi jinsi pekee ya kuhakiksha Waluo wanapata rasilimali za serikali ilikuwa kushirikiana na serikali. Odinga alisongea karibu na Moi, zaidi kuliko wanasiasa wengine. Lakini kifo chake Januari 20, 1994 kilitamatisha ushirikiano huo.

Ushirikiano huo baadaye uliendelezwa na Raila, aliyemrithi baba yake kisiasa. Muda mfupi baada ya kushindwa katika uchaguzi mkuu wa 1997, Raila na Kibaki walitoa taarifa ya pamoja Januari 2. Lakini baada ya siku nne, Raila alitoa taarifa yake akimpongeza Moi kwa ushindi. Akifuata nyayo za 1993-4 za Jaramogi, Raila alibuni mkataba na Moi mnamo Februari 1998, ambapo KANU na NDP zilianza "ushirikiano".

Ni muungano huo ambao baadaye ulivunja Kanu. Wakati wa ushirikiano huo, Moi alimruhusu Raila kununua kiwanda cha mabaki ya miwa mjini Kisumu na baada ya kuvunja chama chake akateuliwa waziri. Ingawa Raila alikuwa na matumaini Moi angemteua kuwa mrithi wake, alishtuka alipomteua Uhuru Kenyatta. Lakini alikuwa amefaulu kuzuia kutengwa kwa Luo Nyanza.

Raila alirudia ujanja huo katika mwafaka maarufu kama handisheki alipofaulu kuanzisha mpango wa kufanya kazi na Rais Kenyatta. Kwa mara nyingine, Raila, licha ya kuwa katika upinzani, alicheza karata zake vizuri. Dkt Ruto akiwa mamlakani sasa, inasubiriwa kuonekana jinsi Raila na wafuasi wake wataendesha siasa zao na iwapo watajadiliana naye ili wapate nafasi serikalini.

***jkamau@ke.nationmedia.com @johnkamau1***

*-- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# habari kwa picha



Waokoaji wakiondoa mwili wa mwathiriwa aliyekufa katika ajali ya ndege ya kampuni ya Yeti Airlines iliyoanguka katika eneo la Pokhara, mnamo Januari 16. Nepal iliadhimisha siku moja ya maombolezi kwa waathiriwa wa mkasa mbaya zaidi wa ndege kuwahi kushuhudiwa nchini humo kwa miongo mitatu huku watu 67 wakithibitishwa kufa katika ajali hiyo. PICHA | AFP



Jumba la Wizara ya Fedha jijini Washington, DC, mnamo Januari 18. Waziri wa Fedha wa Amerika Janet Yellen alisema nchi hiyo ilitarajiwa kufikia kiwango cha juu zaidi cha mikopo kinachokubalika kisheria mnamo Alhamisi. PICHA | AFP




Marc Angel (katikati) wa Luxembourg akipongezwa baada ya kuchaguliwa Makamu-Rais wa Bunge la Ulaya mjini Strasbourg, mashariki mwa Ufaransa, mnamo Januari 18. PICHA | AFP




Jamaa wa mwanaharakati wa LGBTQ Edwin Kiprotich Kipruto, maarufu kama Chiloba, ambaye mwili wake uliwekwa ndani ya sanduku na kutupwa kwenye barabara Kaptinga-Kipkenyo Kaunti ya Uasin Gishu, na waombolezaji wengine wakitazama mwili wake wakati wa ibada ya mazishi eneo la Sergoit, Kaunti ya Elgeyo Marakwet, mnamo Januari 17. PICHA | JARED NYATAYA



Mfanyakazi akiwasilisha picha ya Mtaliano mwigizaji wa Hollywood marehemu Gina Lollobrigida kuwekwa karibu na mwili wake katika Capitoline Hill, mjini Rome, mnamo Januari 18. PICHA | AFP



Helikopta ya Ukraine kiachilia wingu la vifusi kama mojawapo ya mbinu ya kujikinga na makombora huku ikiruka kwenye anga ya mji wa Bakhmut, eneo la Donetsk, mnamo Januari 17. PICHA | AFP



Wakimbizi wa ndani wakibeba makaa kutoka msituni karibu na mlima wa volkeno wa Nyiragongo katika Hifadhi ya Kitaifa Virunga, DRC, mnamo Januari 13, kufuatia kuzuka upya kwa uasi wa wanamgambo wa M23 kaskazini mwa jiji la Goma. PICHA | AFP

Nation Media Group "ePaper Copy"

Jukwaa La Vijana



# HATUA KUBWA MBELE

*Kupitia ubunifu wake wa jukwaa la simu, Duhqa, Victor Maina anaweza kupelekea wateja bidhaa popote walipo kwa haraka na bila gharama zaidi*

NAFASI YA VIJANA

# Jinsi vijana wanaweza kufaidi ajira za kaunti

**Mpango wa makao:** Miradi hii ni baraka na mchango wake kwa taifa zima hauwezi kukisiwa

• NA MOSES OJUANG'

Nchini Kenya, chaguzi hazimaliziki. Daima huwa kuna hali ya kampeni inayoendelea muda mrafu baada ya muhula kumalizima. Wakati ambapo wanasiasa wanang'ang'ania nyadhifa kuu za kujifaidi kiuchumi, lugha wanayotumia ya kujisifu huwa na ushawishi mkubwa na inayojumuisha eneo zima wanalosimamia. Huwa wanatumia "Sisi" mahali ambapo wanafaa kusema "Mimi." Huu ni ukweli wa sifa yetu na ndicho kiini cha migogoro katika kaunti nyingi kama vile Meru, Kericho, na nyinginezo ambako viongozi bado wanagombana huku umma ukibaki kutazama.

Mivutano kuhusu mamlaka pia inaendelea katika serikali kuu lakini ni lazim tukubali kuwa afisi ya rais tayari imemakinika vilivyo katika juhudi za kutimiza ahadi ilizowapa wapiga kura wakati wa kampeni kali mwaka uliopita. Mnamo Oktoba mwaka jana, Rais Ruto alizuru Kaunti ya Homa Bay. Ni wakati ambao viongozi wa eneo hilo walikuwa bado na machungu moyoni na hawakuwa wamekubali kwamba hawakushinda urais. Matokeo ni kuwa wengi wao walipuuza ziara ya Rais.



Hakufa moyo na mwaka huu hatimaye alirudi huko na kupokelewa kwa shangwe na nderemo. Ujumbe wa kisiasa kwa watu wa eneo hilo ni kwamba yeye ni rais wa Kenya wala si kiongozi wa wananchi waliompigia kura pekee. Ujumbe huo ulieleweka na ukapokelewe vyema.

Kando na aina hiyo ya mapinduzi ya kisiasa, ni ukweli kwamba alikuwa na ajenda ya kiuchumi ambayo tuna hakika itachochea maendeleo katika kaunti hiyo.

Miongoni mwake ni kukamilishwa kwa miradi ya barabara ambayo tayari ilikuwa imeanzishwa lakini ikakwama; ujenzi wa soko la kisasa na makao ya gharama nafuu kwa wakazi mjini Homa Bay.

Miradi hii ndiyo muhimu zaidi kwa kaunti hiyo na itafungua maendeleo makuu kiuchumi ambayo yamelemazwa na ukosefu wake.

Hii ndiyo fursa hasa ambayo vijana wa Homa Bay wamekosa kwa muda mrefu. Wavuvi kwenye fuo za ziwa, wanaochukua zaidi ya saa 12 kufikisha bidhaa zao sokoni, sasa itawachukua chini ya saa moja kusafiri umbali huo huo na kupata faida kutokana na jasho lao.

Ujenzi wa nyumba 5,000 za gharama nafuu mjini humo, kando na kutoa ajira kwa vijana, utavutia biashara nyingine kama vile uvunaji wa mchanga, uundaji wa matofali na uchukuzi wa bidhaa za ujenzi.

Nafasi za ajira kutokana na ujenzi huo zitaboresha hali ya maisha katika kaunti nzima. Rais alimshauri mwanakandarasi aliyeteuliwa kuajiri wafanyakazi kutoka miongoni mwa wakazi wa Homa Bay na pia kutumia bidhaa za ujenzi kutoka eneo hilo kwa sababu ziko.

Hatua hii huenda ikamaliza kuongezeka kwa mitaa ya mabanda mjini Homa Bay. Familia nyingi zilizolemewa kifedha mjini Homa Bay huishi kwenye mitaa ya mabanda ya Shauri Yako, Makongeni, Sofia na Misita. Wanaishi katika vibanda vilivyojengwa kwa mabati yaliyochakaa.

Kwa vijana wenye bidii wa kaunti hiyo, hii ni fursa ambayo hawafai kupoteza. Tunajua kuhusu kazi ya sulubu wanayofanya ili kupata riziki, wanachopata kutokana na jasho lao hakifai kamwe.

Wanaochimba mchanga, kwa mfano, hupakia tani za mchanga kwenye malori kwa malipo duni; watengenezaji matofali hufanya kazi kwa majuma kadhaa na kuishia kuuza tofali moja kwa Sh4 kwa sababu tu hawawezi kufikia soko kwa hivyo wanatumiwa vibaya na mawakala. Tabia hiyo ni lazima ikome.

Miradi hii ni baraka kubwa na mchango wake kijamii kwa kaunti nzima hauwezi kukadiriwa.

Hakika, ni matumaini yetu ya dhati kwamba maendeleo hayo yatatekelezwa katika kaunti zote nchini. Kwa njia hiyo, huenda tukaona mabadiliko makubwa katika maisha ya wananchi.

*Bw Ojuang' huandika kuhusu masuala ya kijamii.*

***mojuang@gmail.com***

*Una maoni yoyote kuhusu masuala ibuka? Tungependa kusikia kutoka kwako. Tuma maoni yako kwa:* ***weeklyreview@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

## WANAVYOSEMA



**Jedidah Mwongeli**

Ziara ya Rais William Ruto katika ngome ya upinzani eneo la Nyanza ni ishara ya ukomavu wa demokrasia ambao umetoa nafasi ya kumuisha watu wote. Rais aliweza kuketi na viongozi wa eneo hilo kujadili ajenda ya kubadilisha uchumi. Hii ni hatua muhimu katika kufanikisha utangamano wa kitaifa kupitia mazungumzo na wale tunaotofautiana nao.

***- Afisa Mkuu wa Utekelezaji, Landscape Kenya Foundation***



**Joseph Owino**

Ziara ya siku mbili ya Rais Ruto katika eneo la Nyanza, ambalo lilimpigia kura kwa wingi mpinzani wake katika uchaguzi wa Agosti 2022, ni hatua ya busara. Kiongozi wa Taifa ana uhuru wa kuzuru pembe zote za nchi na kutokana na weledi wake wa kisiasa, alitumia fursa hiyo kuzindua miradi kadhaa ya maendeleo ili kuvutia eneo hilo upande wake. Ni wakati tu utadhihirisha ukweli wa mambo.

***- Seneta wa Vijana Kaunti ya Siaya***



**Margaret Muchoki**

Ziara ya Rais William Ruto katika eneo la Nyanza inaonyesha kujitolea kwake kufanya kazi na Wakenya wote. Hatua hiyo itaimarisha uhusiano bora miongoni mwa Wakenya na kushinda ukabila. Ziara hiyo pia inaonyesha nia njema ya kisiasa kutoka kwa serikali na kuangamiza ukabila. Isitoshe, inaonyesha azma ya serikali ya kuendeleza eneo hilo. Ni ishara ya ukomavu wa kisiasa na inapaswa kuhimizwa.

***- Naibu Rais, Muungano wa Chuo Kikuu cha Daystar***



**Daniel Kiptanui**

Kila mara unapokabiliwa na mpinzani, mshinde kwa upendo. Ziara ya mbwembwe na vifijo ya William Ruto katika eneo la ziwa inalenga kuleta taifa pamoja. Kauli ya kwanza iliyotolewa na Rais ilikuwa kushukuru watu kwa kura walizompa na kwa kudumisha amani.

***- Rais wa Wanafunzi, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Bonde la***

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

MTAZAMO WANGU

# JANGA LA MITANDAO YA KIJAMII

**Chunga watoto wako:** Usiwape simu za kisasa…Kama mzazi, ni jukumu lako kuchelewesha iwezekanvyo watoto kuingia katika tovuti za kijamii



NA WAGA ODONGO



Mwezi uliopita, nilisoma hadithi ya kuogofya. Ilihusu msichana wa umri wa miaka tisa ambaye alipanda juu ya kasha huku ndugu yake mwenye umri wa miaka mitano akitazama, akafunga shingoni nyororo ya chuma ya mbwa na akaitundika karibu na bawaba ya mlango iliyokuwa karibu kisha akabembea.

Msichana huyo alikuwa akijaribu kuiga utani wa kuzimia, ambapo watoto ulimwenguni walikuwa wakijinyima pumzi kwa kutumia vifaa vya nyumbani hadi wanazimia ili kurekodi msisimuko wa homoni ya adrenalaini unaotokana na kurudiwa na fahamu.

Tukio zima lilinanaswa kwa kamera huku video inayorekodiwa ikisambazwa kwa mitandao ya kijamii watu wote watazame. Kwa bahati mbaya, kwa baadhi yao igizo hili limewapelekea kurekodi kujiua kwao wakitumia simu zao.

Msichana huyo raia wa Amerika katika hadithi hiyo alifariki saa chache baada ya kutazama igizo hilo. Wiki chache zilizotangulia, msichana raia wa Italia, 10, alikuwa amejaribu igizo sawa akitumia taulo naye pia akafa.

Igizo la utani la kuzimia limeua watoto 15 kwa muda wa miezi 18 huku tovuti za kijamii zikiamua kutumia timu za watu kuchunguza video ambazo zinasambazwa kwa wingi kusimamisha ajali kama hizo. Intaneti ina vitu vizuri; Intaneti ina vitu vibaya. Na imetuteka na kuwa uraibu.

Uraibu ni hali ya kushindwa kuacha kutumia kitu au kufanya jambo hata kama unajua wazi linasababisha madhara.

Sidhani nasumbuliwa na uraibu mkubwa. Sinywi pombe, ninakunywa kawaha vikombe visivyozidi vitano siku ikiwa mbaya zaidi na nafikiri kamari ni ya wajinga. Hata hivyo, napenda YouTube. Siwezi kuacha kuitazama. Ninatazama video za historia kila wakati bila kukoma kupoteza muda mdogo nilionao duniani.

Ninapoandika Makala hii, kompyuta ninayotumia ina hati inayozuia video zote za YouTube kucheza. Imefichika na haiwezi kupangwa upya hata nikifuta brosa. Ili kuiondoa, ni lazima nianzishe upya mfumo wote. Jinsi bora na ya pekee kunifanya nikome ni kuhakikisha hata hakuna njia ninayoweza kuichagua.

Kihistoria, tumetumia njia za habari ambazo ni sawa. Vitabu vina kurasa chache; runinga haikuwa saa 24. Lakini sasa tuna njia za habari ambazo hazina mipaka.

YouTube inakufungulia video inayofuatia mara moja, mitandao ya kijamii ina orodha isiyoisha kila video ikiashiria kuwa tamu zaidi. Kilele kiko mbali kidogo na unaweza kukifikia ukiendelea kutafuta. Silika zetu zilizonolewa milenia moja iliyopita sasa zimeshindwa, hazikuandaliwa kwa wingi usio na mwisho.

Simu zetu zinatupatia mbubujiko usio na mwisho wa msisimko, wote ukinuiwa kutoa kiwango cha juu cha raha akilini zetu. Na kinatuumiza. Mitandao ya kijamii inafanya watu kuwa na wasiwasi, wenye hasira na kujitenga. Ukweli ni kuwa tovuti hizi ni vigumu kuzisimamia. Ikiwa inaweza kuzuia semi kama Instagram ilivyojaribu na hashitegi zinazokosesha hamu ya chakula, watu wanaanza kutumia zilizoandikwa visivyo ili kuingia katika mifumo na kuifungua.

Video nazo, zinahitaji watu wa kuzitathmini, jambo ambalo ni gumu kwa sababu watumiaji ni mamilioni. Nchini Amerika, kiwango cha kulazwa hospitalini cha wasichana baada ya kujaribu kujiua kimeongezeka kwa asilimia 67 tangu 2009.

Huwezi kuhusisha hili na kudorora kwa jumla kwa uchumi duniani kwa sababu ingekuwa hivyo, idadi ingepungua uchumi unapoimarika. Viwango vya kujaribu kujiua vinaongezeka kwa sababu ya tovuti za kijamii ambazo zimehujumu heshima ya wanawake.

Sasa hulinganishwi na msichana jirani, lakini na wanawake warembo zaidi ambao wataalamu wa upasuaji wameunda wameunda.

Watoto nao wanashirikishwa kutazama video kutoka kwa matapeli kujaribu maigizo ambayo ni hatari na kizuri wanachopata ni kulazwa hospitalini. Ninawaza kuwa kama watu wazima hupambana na mitandao ya kijamii, basi athari zake lazima ziwe mbaya zaidi miongoni mwa watoto.

Mitandao ya kijamii inayounganishwa na mingine haijatimiza miaka kumi kwa hivyo, bado hatujajua athari zake kamili kuhusu itakavyokuwa kwa kizazi ambacho hakijui maisha yalivyokuwa kabla ya intaneti.

Apu hizi zinavutia kwa watoto. Tovuti moja ya kijamii ilivutia sana hivi kwamba serikali ya China iliagiza walioiunda wawe wakikumbusha watumiaji kupumzika na kufanya mazoezi.

Kwa bahati mbaya maelezo yanatoa mawazo ya kijinga na changamoto kwa watoto wachanga kuweza kufahamu kikamilifu hatari inayowakabili kwa kushiriki.

Sadifa ni kuwa sheria za data za kibinafsi zinaharibu mambo hata zaidi. Wasichana wawili niliotaja walikuwa wadogo sana kuwa katika TikTok na wangezuiwa kujiunga kwa kutumia programu ya kuzuia umri. Kuna programu zinazokadiria umri kupitia uso. Sheria katika nchi za Ulaya huzuia ukusanyaji wa data za watoto, kumaanisha kuwa, kisheria, huwezi kuchukua na kuhifadhi picha zao ili kuzilinganisha na za wengine.

Kwa hivyo, tuna visa ambavyo watumiaji wanaulizwa kuweka umri na watu wenye umri mdogo wanaweza kuunda akaunti.

Ni ushindani kati ya faragha na usalama. Ili kuwa na amani, nilipiga picha uso wangu kuitumia katika apu moja ya crypto, badala ya kutumia nenosiri ya maandishi. Ninaweza kuchagua kuvamiwa zaidi faraghani na pesa zangu kidogo au ninaweza kudumisha faragha yangu na kusubiri vijana wa Mulot kudukua kadi yangu ya simu na kunipora kila kitu.

Kama taifa, tunahitaji sera kuhusu matumizi ya mitandao ya kijamii kwa watoto. Kama sehemu ya Sheria yetu ya Ulinzi wa Data, tunahitaji kuunda njia za kulinda watoto wanapotumia mitandao ya kijamii.

Hatimaye, suluhu ya mwisho ina wazazi. Hakuna anayeweza kulinda watoto wako kama wewe. Simu ya kisasa pengine inafaa kuwa ya watu wazima. Kama mzazi, ni jukumu lako kuchelewesha sana iwezekanavy, kuwaingiza watoto wako katika mitandao ya kijamii.

***Bw Odongo ni mhandisi wa programu***
***wagaodongo@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

KAZI YA KIPEKEE

# SAFARI YA UFANISI




Erick Wokabi ndiye mmiliki wa 'Carnversations', mmojawapo wa mitandao ya YouTube inayokua kwa haraka kuhusu magari akiwa na wateja zaidi ya 120,000. PICHA | EDDY ASHIOYA

## Erick Wokabi amejitafutia kazi nzuri kutokana na kupenda magari maisha yake yote kupitia Carnversations, mtandao wa YouTube unaohusu magari tu

• NA EDDY ASHIOYA

Kwa aliyepewa kingi - nisimamishe kama umewahi kusikia msemo huu - kingi kinatarajiwa kutoka kwake. Lakini kabla ya kupewa kingi, karibu akipokonywe. Karibu achukuliwe. Hadithi inaanza hivi: alikuwa na umri wa karibu miaka mitano wakati huo, mtoto mwenye matatizo ya kupumua. Siku moja, mtu alikuwa akivuta sigara karibu na nyumba yao. Alivuta moshi huo.

Kumbuka sheria ya Tatu ya Newton: kwa kila kitendo, kuna kinyume sawa. Lakini wakati huu hakuweza kutoa nje moshi huo. Aliugua ghafla. Ilikuwa saa moja jioni, anakumbuka ulikuwa mwaka wa 1999 baada ya Yesu kuzaliwa na magari yalikuwa machache na vigumu kupatikana. Hangepata moja la kumpeleka hospitali. Mama yake mpendwa, na mwanawe akikodolea kifo macho, alimfunga mgongoni na kutembea hadi hospitalini, "umbali wa kilomita kadhaa". Jinsi anavyozungumza kumhusu, unahisi siku hiyo alionekana kuepuka kifo kwa kukataa kwamba kinaweza kutokea.

Inatosha kusema, alinusurika. Alipokuwa akitoka hospitalini, wazo lilimjia: "Kama mama angekuwa na gari, hangepitia yote hayo." Kwa hivyo, mvulana atafanya nini? Mvulana anaamua kumnunulia mama yake gari. Na kwa bahati nzuri, anaona shindano la 'Shinda Gari' likiwa na magari saba, si moja au mawili, ya kushindaniwa. Waandishi wa mswada huo hawawezi kusema hawakujaribu. Oh, na gari lenyewe? Lilikuwa Daewoo Cielo 1300cc, hutahukumiwa ka hujawahi kusikia kulihusu. Ni gari maarufu, kama alivyo yeye sasa.

Anaitwa Erick Wokabi, mwenye umri wa miaka 29 na mmiliki wa Carnversations, mmojawapo wa mitandao ya YouTube inayokua kwa haraka kuhusu magari. (Nilipoandika alikuwa na wateja 120K) "Nafikiri kitu pekee ambacho nimefanya ni magari," ananiambia tukinywa kahawa katika Valencia Gardens kwenye barabara ya Riara. "Ni biashara ghali sana, na unahitaji washirika wenye nguvu kukusaidia."

Ili ufaulu katika ulimwengu wa matini, lazima uwe thabiti. Ina maana ni lazima upate watu ambao watakupa magari kila wiki. Alipata mshirika kama huyo ambaye ni MotorHub, anakopata magari naye anayatangaza na kutaja kampuni hiyo.

Akiwa na digrii ya Kilimobiashara, Uchumi na Usimamizi wa chakula kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo na Tekinolojia cha Jomo Kenyatta, Wokabi alikuwa akitamani kufanya kitu tofauti. Hakutaka kazi za ofisini, ananiambia, akikata moja ya simu anazopigiwa katika simu zake mbili za mkononi. Naona ni mtu mwenye shughuli nyingi. "Shida ni kwamba katika ulimwengu huu, wakati mwingine ni lazima ujifunze kupitia hali ngumu. Tofauti na shule, katika ulimwengu wa magari unafanya mtihani kwanza, kisha unasoma."

Mtihani anaozungumzia ni kuhusu alivyojitosa mara ya kwanza katika biashara ya magari. Alianza kwa kuandika katika Facebook kuhusu magari. Alijua magari jinsi mtu anaweza kujua kila mchezaji wa timu ya kandanda anayopenda - pamoja na wafanyakazi wasaidizi wote.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

Hatimaye mama yake aliponunua gari - Datsun rangi ya kijani kibichi– alijawa na furaha. Anasema ndoto yake ilikuwa kuwa rubani, lakini si madereva pia ni marubani ardhini? Kwa hivyo, alijifunza jinsi ya kuendesha magari kupitia utundu. 'Kutazama na kufanya makosa' ndiyo maneno halisi aliyotumia, lakini Shakespeare alisema nini? Waridi hata kwa jina lingine?

Erick alianza jamii ya magari aina ya Toyota Hiace Kenya. "Ambayo bado ipo," ananihakikishia. Alichapisha vitabu vya mtandaoni kuyahusu na kuuzia wateja wake ambao walikuwa wamefahamu kupitia Facebook au kwa kumsikia. "Nilipata pesa nyingi. Siku moja nilipata Ksh30,000 chini ya saa tatu." Umaarufu wake ulienea kama moto unaochoma nyumba, la, kama injini inayowaka moto.

Bila kujua, juhudi zake zilikuwa zimevutia watu wengine, ambao walimtafuta, wakita afanye kazi katika biashara zao. Ni wakati huo ambapo alijifunza kazi akiendelea kujenga jamii yake. Daima mwenye maono, tayari alikuwa ameona mbali. Maisha ya baadaye yalikuwa katika mtandao.

"Niliomba likizo kutoka ofisini na nikaomba Landcruiser kwenda katika mashindano ya magari ya Elgon Challenge." Shida pekee ilikuwa, gari alilokuwa ametambua lilikuwa limeuzwa siku iliyotangulia. Lakini washindi hawana visingizio washindani wao wanapoanza kucheza mchezo. Alitumia alichobahatika kupata. "Badala yake tulipewa Vanguard. Hio ilikuwa wazo baya lakini tulifikiria kwa nini tusilitumie? Tulichunguza gari hilo wakati wa shindano na tukapata ripoti nzuri." Tuliyotaka tulitimiza.

Huku mtandao wake ukiimarika, Eric alichukua hatua iliyofuata. Kuajiriwa hakukukimpa uhuru na alitaka kuwa na nafasi zaidi. Wakati wa kilele cha Covid-19 aliacha kazi yake ya kila siku. Hakumwambia yeyote. Isipokuwa Ibrahim, ambaye kwa wakati huu ni mshirika wake wa kibiashara. "Kunasa filamu sio rahisi, Ibrahim alikuwa na vifaa; nilikuwa na matini," ilikuwa ndoa iliyopangwa mbinguni? Ni kweli. Yaliyofuata ni historia.

"Kuanzia mwaka huu, tutafungua mtandao wa pili kwa watu ambao hawawezi kumudu magari haya yaliyotumika nchi za nje.""Timu yetu ni kubwa sasa," anasema. "Tuna wanasheria, idara ya uhasibu, na ya kiufundi na uhariri." Ananiambia amekataa kazi chache kubwa, akihofia masharti yanayofanana na ya kujifunga ya China yanayopendekezwa. "Ukitaka kujiunga na Carnversations, tunataka kujua kwamba unapenda kitu unachofanya. Hatutaki uhisi kama unakuja kufanya kazi."

**Kumbuka sheria ya Tatu ya Newton: kwa kila kitendo, kuna kinyume sawa. Lakini wakati huu hakuweza kutoa nje moshi huo. Aliugua ghafla. Ilikuwa saa moja jioni, anakumbuka ulikuwa mwaka wa 1999 baada ya Yesu kuzaliwa na magari yalikuwa machache na vigumu kupatikana. Hangepata moja la kumpeleka hospitali. Mama yake mpendwa, na mwanawe akikodolea kifo macho, alimfunga mgongoni na kutembea hadi hospitalini, "umbali wa kilomita kadhaa"**

> **Nahitaji mabawa. Huwezi kuwa muundaji wa matini milele: Hatutaki kuwa wazee waliokataa kubadilika. Tunataka kulea wengine kuwa warithi wetu. Unajua, kuna watu wanaokuwa wachanga na bora. Hiyo ndiyo CSR bora tunayoweza kufanya.**
>
> Erick Wokabi

Kama njia ya kutoka ahadi hadi nchi ya ahadi inaonekana nzuri, nimekosea - nisamehe, kwa sababu haikuwa hivyo. Amekuwa na matatizo yake, hata alikuwa karibu apeane kampuni yake. Ninadadisi zaidi. "Watu walitujia na kutuomba tuwafanyie kampeni ya wiki nane. Ilionekana nzuri sana hadi tulipoipeleka kwa utafsiri zaidi. Walikuwa wameweka sharti fiche kwamba wangemiliki haki za kumiliki matini na kumiliki mvumishaji milele.. kwa ufupi, mradi tu wamekulipa, wanakumiliki." Tuliwataka wabadilishe vipengele hivyo na wakasema havikuwa vibaya. "Ni kielezo tu," walisema. Wakili wetu aliwapuuza. Kandarasi, anasema, huwafunga wahusika.

Alipoacha kazi wakati wa kilele cha Covid, Erick alijifunza mambo machache, baadhi ambayo, wewe, pia, unaweza kuwa ulijifunza. "Hakuna kinachopatikana kwa urahisi. "Usiwe mtu wa kukasirika haraka." Kama unapenda unachofanya, msukumo utakufanya uendelee hata wakati mambo si mazuri."

Anasema gari zuri ambalo amewahi kuendesha kufikia sasa ni [Mercedes] G-Wagon. "Ni gari ambalo kufikia sasa linakupa mseto nadra sana. Ni gari linaloweza kuendeshwa katika barabara isiyo na lami, gari la michezo na pia gari la kawaida, utatu mwafaka. Nililiendesha na nikahisi limenifurahisha sana. Ni gari zuri." Mtoto wa kati aliye na kaka mkubwa na dada mdogo ni mwanamilenia lakini pia anakosoa magari ya kisasa. "Hayo si magari." Basi anapenda gari gani? "BWM E30. Hasa iliyo na milango miwili. Iliyotengenezwa kati ya 1986 na 1995." Au Toyota Landcruiser 80 series. Anapozungumza kuhusu magari, unaweza kuona macho yake yakimetameta. Ninaweza kutambua sura hiyo, ni sura unayoona katika makanisa yenye mvuto kiroho, sura ya mtu aliyejawa na furaha.

Kwake, gari ni zaidi ya mwendo. Ni kipande cha sanaa. "Unafaa kuendesha gari na ufurahie kuliendesha." Kwa wakati huu, anaendesha gari aina ya Subaru Legacy RS, limited edition. "Hili ndilo gari lililofanya Subaru kuwa ilivyo leo." Anaendelea kunifunza kwa nini Subaru ilipakwa rangi ya bluu, kwa sababu ilikuwa ikinufaisha Subaru katika WRC kwa kingo zake za dhahabu. "Sio gari linalotumia mafuta kidogo lakini ni raha kuliendesha. Hilo ndilo gari ninaloendesha nikitaka mwendo wa kasi." Na kwa usafiri wake wa kila siku? Anatumia Volvo S40 iliyoundwa 1998 – ya kijani kibichi.

Je, mambo yamemwendea alivyotarajia akiwa na umri wa miaka 29? "Sisi sote kuna vitu tulivyotaka kufanya tulipomaliza chuo kikuu. Unajua, kupata mke, na watoto na kuendelea. Kwangu mimi, bado. Anachotazama pekee ni siku zijazo. Anataka kupata leseni ya kuendesha ndege za kibinafsi. "Nataka kuwa na mabawa," ndivyo anavyoieleza. Changamoto kubwa kwake ni kuendesha ndege. "Huwezi kuwa muundaji wa matini milele. Hatutaki kuwa wazee waliokataa kubadilika. Tunataka kulea wengine wawe warithi wetu. Unajua, kuna watu wanaokuwa wachanga na bora. Hiyo ndiyo CSR bora tunayoweza kufanya."

Ilimgharimu nini kutimiza malengo yake? "Kufanya kazi usiku. Kufanya kazi katika maeneo yasiyo ya kawaida, lakini tumefurahia chochote ambacho tumefanya." Kama hufurahii unachofanya utakiacha haraka. Anazungumzia kwa upendo mkubwa East African Safari Classic, ambayo Carnversations ilikuwa mshirika rasmi. Anatazamia kujiunga na mbio za magari kama dereva. Lini? Hivi karibuni. "Kazi hii itakuharibia mahusiano usipopata watu wanaokuelewa. Wakati mwingine unaacha maisha ya kijamii." Ananieleza kisa ambapo alilazimika kufuta miadi kwa sababu alilazimika kurudia kunasa video baada ya kupoteza sauti.

Kuwa maarufu kunakupa mambo mengi, lakini pia kunakupokonya kitu. Hasa wakati umaarufu unatokana na kipawa chako, kutoka kwa kitu ambacho umekuza na kupenda. Watu humsimamisha barabarani kila mara kumuuliza maswali kuhusu magari. "Hawa ni watu ambao hawataelewa wakati umechoka." Ni tunda lenye sumu.

Anawezaje kuelezea ufanisi? "Kuwa bora kuliko ulivyokuwa jana." Anasema mwongozo wake wa kila siku ni Kai Zen, filosofia ya Wajapani ya kuwa bora leo kuliko ulivyokuwa jana. Pengine inaeleza ni kwa nini anapenda kuendesha magari kutoka Japan.

Kati ya sehemu zote za gari, angetaka kuwa nini? "Injini. Unataka kukimbia na kuwa chanzo cha nguvu. Mshumaa unaowasha mingine." "Sijuti kutumiwa katika miaka yangu ya mwanzoni," anasema. "Leo naichukulia kama karo ya shule. Hiyo ndiyo gharama niliyolipa kujifunza na kufika nilipo."

Hiyo inanikumbusha msemo mwingine wa Asia - Kintsugi – sanaa ya Japan ya kuunganisha vipande vilivyovunjika pamoja na dhahabu, kujenga wazo kwa kukumbatia dosari na makosa, unaweza kuunda picha maridadi zaidi.

***eddieashioya@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "ePaper Copy"

BIASHARA REJAREJA

# UUZAJI MAMBOLEO

**Duhqa, apu ya simu ya mkononi ya kuuza bidhaa zamatumizi zinazonunuliwa kwa wingi, inawezesha wafanyabiashara kutafuta bidhaa kwa urahisi na kupelekewa kwa muda mfupi bila malipo**

• NA NDUGU ABISAI

Ilimvutia sana. Moyo wa biashara. Mnamo 2019, katika joto la Mombasa, Victor Maina alibuni wazo: kuuza maji safi ya kunywa ndani ya karatasi zisizoharibu mazingira. Wakati huo, alikuwa akifanya kazi na kampuni ya kusafirisha mizigo ya kimataifa, kwa hivyo uuzaji ulikuwa ukitembea katika mishipa yake kama damu.

Aliungana na rafiki yake, Dudu Moilwa, na kwa maneno ya Victor, biashara ilikuwa ikifanya vyema miaka miwili baadaye, walipoamua kuiuza kwa mwekezaji Mombasa walipogundua pengo lingine katika soko. Wakishirikiana na rafiki yao, David Angweny, walianzisha Duhqa, jukwaa la biashara-kwa-biashara la kusambaza bidhaa za matumizi zinazonunuliwa kwa wingi. Hiyo ilikuwa Januari 2021.

Duhqa ina apu ya simu inayowezesha wafanyabiashara kununua bidhaa kutoka kwa watengenezaji kwa idadi inayowafaa, na kupelekewa katika muda mfupi, na bila malipo, hadi walipo, na hivyo basi kupunguza gharama ya kufanya biashara kwa karibu asilimia 15-20.

Kariuki Maina, mchuuzi wa chakula katika barabara ya River Road, ni mtu mwenye furaha. "Nimeuza smokie na soseji kwa miaka 11 iliyopita. Wakati huo wote, nilikuwa nikienda madukani kununua bidhaa mimi mwenyewe, jambo linalotumia muda ambao ningetumia kwa uuzaji. Baada ya kupakua apu hiyo kwa ushauri wa rafiki anayefanya biashara hii, kazi yangu imekwua rahisi. Huwa naagiza bidhaa na wananiletea ndani ya saa mbili au tatu bila kuniongezea gharama. Duhqa hufanya kazi yangu kuwa rahisi," anaeleza.

Je, Victor na marafiki zake walifanya nini kuanza biashara hii? "Mwanzoni, tuliweka pesa zetu ili kupata wateja. Kisha ulifikia wakati ambao tulihisi tulihitaji kupanuka nchini na kikanda. Biashara ilikuwa ikipanuka kila mwezi na tulihitaji kudumisha ukuaji huo. Wakati huo tulijiunga na Techstars kundi la Accelerator Oktoba 2021. Tuliomba mtaji wa dola milioni mbili, ambao tulipewa baada ya ukaguzi mkali na mafunzo," anasema Victor.

Kwa ufadhili huo, walipanua shughuli zao kutoka maeneo mawili - Nairobi na Kati ya Kenya - hadi sehemu za Mashariki ya Kenya, pembeni mwa eneo la Pwani kama Voi na Taita Taveta, na sasa wameanza kupenya Kaskazini ya Kenya, wakiwa wameuzia wafanyabiashara kaunti ya Garissa.

Duhqa imevuka mipaka ya Kenya pia, huku Madagascar ikiwa eneo jipya inayolenga. "Sababu yetu kukubali Madagascar ni kuwa ina soko kubwa ya kipekee kama letu. Mitaa ya mabanda huko inakumbwa na usambazaji duni wa bidhaa kutokana na changamoto kama barabara mbaya, uhaba wa mtaji na ukosefu wa usalama. Kwa kuwapa jukwaa kama hili, tunawawezesha kupata bidhaa bila kutatizika," anaeleza Victor. Pia wamepenya Canada, Rwanda na nchi jirani ya Uganda. Kwa wakati huu, Duhqa inahudumia wafanyabiashara hai 8,791 ikiwa imesajili zaidi ya wanachama 10,000 katika apu yake. Wana kampuni 42 za kutengeneza bidhaa pia, ambazo wanaunganisha na wafanyabiashara. "Wanachama hai ni wale wanaoagiza bidhaa angalau mara mbili kwa wiki."




Victor Maina akiwa katika ghala lake jijini Nairobi. Alianzisha Duhqa mnamo Januari 2021. Duhqa ina apu ya simu ya mkononi inayomwezesha mfanyabiashara kuagiza bidhaa kiasi anachotaka kutoka kwa watengenezaji.

Kwa Margaret Aloo, mwenye duka mtaa wa Mukuru kwa Njenga, mtaa wa mabanda jijini Nairobi, biashara ni laini sasa. "Nina duka dogo. Kupata mtu wa kuniletea bidhaa chache katika eneo langu ni vigumu," anasema Margaret. "Duhqa ni wazuri kwa sababu wananipunguzia kazi ya kutafuta bidhaa."

Duhqa pia imekua kwa idadi ya wafanyakazi - kutoka timu ya kwanza ya watu watatu walioianzisha hadi 50 kwa wakati huu. Pia imeongeza maeneo mapya ya kushughulikia ikiwa ilianza na bidhaa za matumizi zinazonunuliwa kwa wingi na kupanuka hadi uuzaji wa bidhaa za kuhifadhi kwenye baridi, kwa kushirikiana na kampuni ya kutengeneza nyama humu nchini. Wakati huu, Duhqa husambaza karibu pakiti elfu moja za soseji kwa wauzaji wa rejareja Nairobi kila asubuhi. Wanauza nyama ya ng'ombe, nyama ya nguruwe na kuku pia.

Mwanzoni, ilikuwa ikichukua siku nzima kupeleka bidhaa kwa wauzaji, muda ambao waliweza kupunguza hadi saa sita. Sasa wanaweza kuahidi kufikisha ndani ya saa mbili.

"ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media



Victor Maina na wafanyakazi wa Duhqa jijini Nairobi. Kuelewa soko kumesaidia kupunguza gharama ya kuendesha biashara yao na ya wateja wao.

"Tunajua matatizo ya wateja wetu. Kuelewa soko kumetusaidia kupunguza gharama ya shughuli katika biashara yetu na wateja wetu," anasema Victor. Wamepanua pia shughuli na kuanza kupelekea wateja bidhaa nyumbani.

Hivi majuzi, Duhqa ilianzisha bidhaa mpya kutokana na maombi mengi kutoka kwa wateja waliokuwa wameuzia nyama. "Wateja walitaka vinywaji vya kuandamana na nyama. Kwa hivyo tuliunda bidhaa inayoitwa Duhqa Party, ambayo apu inapendekeza vinywaji vinavyofaa kwa aina za nyama unayonunua na inakuletea zote pamoja," anaeleza Victor.

**Duhqa pia imekua kwa idadi ya wafanyakazi - kutoka timu ya kwanza ya watu watatu walioianzisha hadi 50 kwa wakati huu. Pia imeongeza maeneo mapya ya kushughulikia ikiwa ilianza na bidhaa za matumizi zinazonunuliwa kwa wingi na kupanuka hadi uuzaji wa bidhaa za kuhifadhi kwenye baridi, kwa kushirikiana na kampuni ya kutengeneza nyama humu nchini.**

Wanaendelea kuunda ushirikiano na taasisi ya kifedha ya humu nchini kuwezesha wafanyabiashara wadogo na wanunuzi binafsi kupata bidhaa kwa mkopo.

"Tunalenga hali ambayo wewe, mnunuzi, unataka dawa ya mtoto wako lakini huwezi kuipata kwa sababu huna pesa za kutosha mkononi. Baada ya kutathmini uwezo wako wa mikopo, tunakuruhusu kupata bidhaa zako kwa mkopo kisha ulipe baadaye kwa masharti tutakayokubaliana. Tunataka kurahisishia watu kununua bidhaa. Lakini zaidi kuwa duka ambalo unaweza kwenda kila wakati ukiwa na pesa au bila," anasema Victor.

Katika ulimwengu unaojaa biashara zinazoanzishwa, ni nini kimefanya Duhqa kufaulu? Kulingana na Victor, ni kufahamu kuwa hawawezi kuwa biashara ndogo milele. Walijifunza hili mapema katika biashara yao na hivyo basi wakatia bidii kufaulu ili waweze kuhakikisha uendelevu wao.

"Tulipoanza, tulielewa kwamba kwa kukidhi hitaji, tungefaulu haraka. Kupata faida kulimaanisha tungepanuka na hivyo ndivyo tuliunda biashara yetu. Tulijua wazi kuwa yetu ilikuwa biashara na tumeisimamia kama biashara," atamatisha Victor.

***nduguabisai@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*


## Baada ya kupakua apu hiyo kwa ushauri wa rafiki anayefanya biashara hii, kazi yangu imekwua rahisi. Huwa naagiza bidhaa na wananiletea ndani ya saa mbili au tatu bila kuniongezea gharama.

Kariuki Maina, mchuuzi




Nation Media Group "ePaper Copy"

maoni




Nation Media Group "ePaper Copy"

■ Kwa umma, polisi ni wezi wanaotumia sare na silaha zao kwa manufaa yao binafsi

# Kwako IG, raia kamwe si maadui wako



KWENDO OPANGA

Aliyekuwa Jaji Mkuu David Magara, aliyeitwa mkora na Rais Kenyatta na Naibu wake William Ruto mwaka wa 2017, alipoanza kazi ya kubadilisha huduma za polisi na magereza, maafisa wanne walifikishwa kortini na kushtakiwa kwa kujaribu kutekeleza wizi wa mabavu.

Runinga ya NTV ilionyesha picha za jaribio la maafisa hao la kuwateka nyara wahudumu wa kituo cha kubadilisha pesa za kigeni. Kisa hicho kilivutia na kushangaza umma uliotazama na wanaolipa ushuru. Kizimbani, maafisa hao wanne walivalia barakoa na anoraki kuficha sura zao kwa umma uliojawa na mshangao.

Jukumu kuu la polisi ni kuzuia uhalifu na kulinda umma dhidi ya wahalifu. Umma utageukia nani kama wahalifu ni maafisa wa polisi wasiovalia sare rasmi? Polisi wakivunja sheria, basi, ninavyosema, hakuna sheria. Maafisa wakitumia silaha zao kuibia umma, basi huduma hiyo inakoma kuwa shirika la kutekeleza sheria, na kuwa mtandao wa wahalifu.

Polisi watafanya kazi yao wakiungwa mkono na umma. Polisi watapata habari kutoka kwa umma kama umma utawaamini nao pia, kuamini umma.

Kama nilivyowahi kusema hapa awali, polisi wanachukulia umma kwa uzuri zaidi kama watu duni na kwa ubaya zaidi kama maadui. Mwongozo wa imani ya polisi ni kwamba adui ni raia.

Hii ndiyo sababu mnamo 2021, vijana waliokuwa wamehitimu mafunzo ya Polisi wa Kukabiliana na Fujo (GSU) walisambaza video punde tu baada ya gwaride ya kufuzu ambayo walionya umma kuhusu jinsi walivyokuwa (sisi ni wazii) na jinsi wangesababisha madhara kwao. Wakuu wao waliofedheheka walitoa taarifa wakikanusha wahitimu hao vijana walikuwa wakielezea maadili ya kikosi hicho. Na walikuwa wakifanya hivyo.

Polisi wanapotazama umma kama adui badala ya washirika wao katika kupigana na uhalifu, basi kazi ya uchunguzi, kukusanya habari za ujasusi na ushahidi na kuzuia uhalifu inakuwa ngumu sana.

Kama imani miongoni mwa maafisa wa polisi ni kwamba umma ni adui, umma nao utaepuka wanaume na wanawake hao wanaovalia sare za bluu.

Kwa umma wa Kenya, maafisa wa polisi ni wezi wanaotumia nyadhifa zao, sare zao, nembo na silaha kwa manufaa yao binafsi, kupuuza umma na kuharibu huduma hiyo na haki.

Kwa umma wa Kenya, polisi wanaume na wanawake ni kikosi cha vitisho, kulazimisha, kugandamiza na kunyanyasa, kinachohudumia na kutetea walio mamlakani.

Kwa maelezo tofauti, kikosi ambacho kililinda Lord Delamere alipowapiga risasi Waafrika kama spoti kutoka Norfolk na Grogan, alipoendesha pikipiki yake Uthiru kwa kasi ya juu, akiogofya Waafrika hadi kifo kwa raha yake, sasa, kwa mujibu wa Rais William Ruto, kinaua na kutupa mili katika Mto Yala. Katika miaka ya 1980, walikuwa wakiwatupa kupitia dirisha za ofisi zao za Nyayo House. Ufisadi katika huduma ya polisi sio tu mfumo, ni taasisi.

Hakika, konstebo katika kituo cha barabarani ni yule yule tu atapanda cheo na kuwa kamanda katika kaunti au makao makuu ya kitaifa. Ni huyo atakuwa Inspekta Jenerali.

Na, sehemu ya hongo inayochukuliwa katika kituo cha barabarani inafika mifuko ya maafande walio katika madawati ofisini.

Si ajabu ajabu basi, ni Vigilance House iliyopinga mengi ya mageuzi yaliyopendekezwa katika polisi kufuatia ghasia za baada ya uchaguzi mkuu wa 2007/08 na ujio wa Katiba ya Kenya 2010.

La mwisho, ambalo linaweza kuwa la kwanza, kwa mujibu wa Rais na Naibu Rais Rigathi Gachagua, polisi wamekuwa wakitumiwa kulipiza kisasi kati ya wanasiasa. Wanasiasa ndio waliomuita aliyekuwa Jaji Mkuu David Maraga mkora.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni

■ VITENDO VYA UHAINI

# Wafunge jela kisha utupe funguo mbali



MACHARIA
GAITHO

Mtu anayeaminika anafaa kutembelea Ikulu na kunong'oneza siri kwa masikio ya Rais William Ruto. Anahitaji ukumbusho wa dharura, kuwa yeye ni Rais wa Jamhuri ya Kenya na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yote ya Ulinzi.

Anafaa kuelewa kuwa yeye si mwanablogu yeyote yule au mwanaharakati wa kisiasa anayetaka kutambuliwa, bali kiongozi ambaye hafai kuonekana akitoa matamshi ya kisiasa kiholela au madai yasiyoweza kuthibitishwa.

Kila kauli anayotoa Rais hadharani lazima ionekane kuwa ya kweli. Inabeba uzito wa uamuzi wa serikali au sera, na mara nyingi huwa ishara ya hatua itakayochukuliwa.

Huu si msimu wa kampeni ambapo wanaotafuta afisi za umma wanaweza kusamehewa wakitoa madai yasiyo na ukweli.

Rais wa Jamhuri anaposimama katika jukwaa la umma na kutangaza kuwa mtu fulani au kundi fulani lilipanga uhaini, mauaji ya viongozi, mauaji ya halaiki, shambulio la kigaidi kwa bomu au uhalifu mwingine mbaya, itachukuliwa kuwa asasi za uchunguzi zimemshauri kufanya hivyo.

Inamaanisha pia kuwa, isipokuwa mshukiwa awe amejificha, basi tayari amekamatwa na anasubiri tu kufikishwa kortini ambako wapelelezi sasa watajaribu kushawishi jaji kwamba, kweli, mshukiwa huyo anafaa kuhukumiwa kifo.

Rais akitoa madai kama hayo hadharani lakini hakuna ushahidi kuwa uhalifu wa aina hiyo ulichunguzwa kikamilifu na washukuwa kuzuiliwa kusubiri kufunguliwa mashtaka, usemi wake hauna thamani bali cheche zinazotolewa kila mara na watu waliolipwa.

Hivyo ndivyo tunavyochukulia madai ya Ruto kwamba kulikuwa na njama ya kumteka nyara na kumuua aliyekuwa mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka Wafula Chebukati ili kumzuia kumtangaza, yeye, Ruto, kuwa mshindi wa uchaguzi mkuu wa Agosti mwaka jana.

Kama kweli kuna ushahidi wa njama kama hiyo, tunaweza kutarajia kwamba leo wahusika wamekamatwa na watafikishwa kortini hivi karibuni.

Tunaweza, bila shaka. Kudhani kuwa watu pekee wanaotamani sana kumzuia Ruto kuwa rais na wenye uwezo wa kupanga mauaji ya mwenyekiti wa tume ya uchaguzi ni wale tu wanaotaka kiti hicho.

Rais anaweza tu kuwa anazungumza kuhusu mtangulizi wake, Rais Uhuru Kenyatta na mrithi ambaye Kenyatta alimpendelea, Raila Odinga.


Huenda kuna wengine waliohusika kama vile aliyekuwa Waziri wa Usalama Fred Matiang'i na maafisa wake katika kitengo cha usalama. Lakini hao watakuwa tu watumishi wa walio na uwajibikaji mkubwa.

Kama, kweli, kulikuwa na njama kama hiyo ya kupindua uamuzi wa wananchi kwa kutumia mbinu katili kama hizo, ni lazimawahusika wakabiliwe na mkono wa sheria.

Itakuwa hatua ya kuchelea kutekeleza wajibu wake kimakusudi, kuruhusu Bw Kenyatta, Bw Odinga na wengine ambao huenda walihusika na vitendo vya uhaini kuendelea na maisha yao ya kawaida, kufurahia ulinzi wa asasi za serikali na kutumia nyumba, afisi, uchukuzi, huduma, chakula na huduma zingine kwa gharama ya umma.

Njama kama zilizodaiwa kupangwa haziwezi kuchukuliwa kwa wepesi. Mtu yeyote aliyehusika katika jaribio la kuvunja sheria na mamlaka ya nchi lazima achukuliwe hatua Washukiwa katika visa kama hivyo lazima wachukuliwe kama wakosaji wakubwa.

Hakuna jinsi waliopanga njama ya kuhujumu kuwepo kwa nchi hii wanaweza kuachwa wakitembea huru, wakifurahia mali waliyopata kwa njia haramu, huku tukipuuza mateso ya walala hoi maarufu kama Mahasla.



**Hilo si suala dogo na lazima lichukuliwe kwa uzito unaostahili. Lakini je, itakuwaje ikibainika kuwa hapakuwa na njama kama hiyo na Rais alikuwa akicheza siasa tu? Jambo kama hilo pia linafaa kuchukuliwa kwa uzito. Rais hafai kujihusisha na mienendo kama hiyo isiyo ya uwajibikaji, hatari na ya kuhadaa bila kukabiliwa na hatari ya kuadhibiwa**

Kenya ni nchi inayoongozwa na sheria. Ni mojawapo la mataifa machache Afrika yaliyobakia huru na kuendesha shughuli zake baada ya kupata uhuru na sasa yanafurahia demokrasia inayonawiri.

Mafanikio haya yaliyopatikana kwa jasho hayafai kudharauliwa. Mtu yeyote anayetishia thamani ya utaifa wetu lazima afungiwe jela na funguo zitupwe.

Habari za mipango chafu kama hiyo zinapotoka kwa mtu kama Rais wa Jamhuri, hatuna lingine bali kuzichukulia kwa uzito kwa sababu ni lazima zinatokana na vianzo vya habari vinavyoaminiwa.

Kwa hivyo, ni wajibu wa kila Mkenya kukamata washukiwa akiwaona na kuwakabidhi kwa walinda usalama. Hilo si suala dogo na lazima lichukuliwe kwa uzito unaostahili. Lakini je, itakuwaje ikibainika kuwa hapakuwa na njama kama hiyo na Rais alikuwa akicheza siasa tu?

Hilo pia linafaa kuchukuliwa kwa uzito. Rais hafai kujihusisha na mienendo kama hiyo isiyo ya uwajibikaji, hatari na ya kuhadaa bila kukabiliwa na hatari ya kuadhibiwa. Huu utakuwa wakati wa kufanyia majaribio vifungu vyote vya kisheria na kikatiba vinavyoharamisha ukiukaji wa mamlaka ya urais.

*** *** ***

Nilisoma kuhusu mcheshi mmoja katika Bunge letu akipendekeza sheria itakayomlazimu kila mtangazaji kucheza nyimbo za kizalendo kabla ya kila taarifa ya habari.

Hilo linaweza kuonekana kuwa pendekezo lenye malengo mazuri, lakini ni la kijinga kabisa. Kuanzishwa kwa msururu wa matangazo ya habari saa 24 kumeifanya vigumu kukadiria wakati taarifa ya habari inaanza kusomwa.

Muhimu zaidi itakuwa usemi wa kale kuwa uzalendo ni kimbilio la mwisho kwa muongo. Wakenya walipigana na kufa kwa ajili ya demokrasia kujinasua kutoka kwa utumwa.

Katika mazingira ambayo walio uongozini mara nyingi hawawezi kutofautisha kati ya uzalendo na uaminifu wa kijinga au uliolazimishwa kwa mtu au chama, sharti kama hilo litakuwa sawa na kuturudisha katika enzi za giza.

*gaithomail@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

SIASA ZA UPINZANI

# KARATA YA RAILA 2023

## Mpango wa Raila wa kutoa ripoti ya "kuaminika" kutbibitisha alishinda uchaguzi wa Agosti unaweza kuonekana kazi bure; lakini inaweza kuwa hatua inayolenga kuendelea kudumisha umaarufu wake unaofifia

NA OSCAR OBONYO

Mgombea urais aliyeshindwa Raila Odinga anapanga kutoa "ushahidi wa kuaminika" kuhusu uchaguzi wa Agosti iliyopita, siku chache tu baada ya Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), anayeondoka Wafula Chebukati, kuzindua ripoti ya utathmini, inayomlaumu Raila kwa "kujaribu kubadilisha uamuzi wa wananchi."

Kutolewa kwa ripoti hiyo ya IEBC kunampa Waziri Mkuu huyo wa zamani nafasi nzuri ya kuelezea ushahidi wake ambao, washirika wake wanadai, ni wa kweli.


Inasemekna kuwa mgombeaji urais huyo wa muungano wa Azimio La Umoja-One Kenya alileta pamoja kundi la wataalamu wa uchaguzi na teknolojia kutoka ng'ambo, ambao, kwa miezi mitatu iliyopita, wamekuwa wakitayarisha ripoti ya ushahidi "kuhusu jinsi uchaguzi wa urais wa 2022 ulivyoibwa" ili kumpendelea mpinzani wake mkuu, William Samoei Ruto wa United Democratic Alliance (UDA).

Kulingana na washirika wake wa karibu, ripoti hiyo, inayosemekana kuonyesha kuwa mgombeaji wa Azimio alishinda uchaguzi huo kwa zaidi ya kura milioni mbili, inaelezea kwa kina jinsi kura za urais zilivyotungwa kidijitali na kwa mikono, kupitia uchapishaji wa karatasi sambamba na za ziada na pia njama za kiufundi katika uwasilishaji wa matokeo.

Hata hivyo, shughuli ya kutayarisha ripoti hiyo imewagawanya viongozi wakuu katika Azimio, baadhi yao wakitaja kuwa yenye gharama kubwa na iliyopitwa na wakati.

Hata kama, kwa mfano, itafaulu kushawishi Wakenya kuwa Odinga alishinda uchaguzi wa Agosti, Ruto, ambaye anashikilia kuwa alishinda "kihalali" hatashawishiwa wala kulazimishwa kuondoka Ikulu. Kando na hayo, Mahakama ya Upeo tayari - kwa haki au visivyo – ilitia tamati suala hilo.

Kwa hivyo, Raila ana nia gani katika mpango wake huo?




Sawa tu na wanasiasa wengi wanaoegemea upande wa chama tawala, Kiongozi wa Wengi katika Bunge la Kitaifa, Kimani Ichung'wa anahisi mpango huo ni njama ya Odinga ya kuendelea kudumisha umaarufu wake "unaofifia polepole." Kulingana na Ichung'wa, kiongozi wa Orange Democratic Movement (ODM) anataka kushikilia "uongo" kuhusu kura zilizoibwa na "matumaini ya uongo" kwamba anajitahidi kupeleka wafuasi wake katika Kanaani ya Kibiblia.

Akimwelezea kuwa "Raila yule tunayemjua", Mbunge huyo anadai kiongozi huyo wa upinzani "anacheza mchezo wake wa zamani" wa kufananisha kila kushindwa kwake katika uchaguzi na wizi wa kura, na kwa njia hiyo kurudisha nchi nyuma.

Kutokana na uzoefu wake mkubwa katika siasa, pamoja na kuungwa mkono na kundi kubwa la viongozi wa kisiasa, Odinga alichukuliwa kwa kiwango kikubwa kuwa mgombeaji mkuu katika uchaguzi wa urais mwaka uliopita - jambo ambalo liliungwa mkono na watafiti wengi wa uchaguzi. Si ajabu basi, k kutangazwa kwa Ruto kuwa mshindi kulipokelewa na watu wengi kwa hali ya kutoamini na kuzua hali ya kukata tamaa miongoni mwa wafuasi wa Azimio.

Tangu wakati huo, kumekuwa na hali ya kutoridhika katika ngome za Raila na kulingana na Profesa Makau Mutua, ambaye alikuwa msemaji wa kampeni yake ya urais, wananchi wamekuwa wakingoja mwelekeo na hatua. Profesa Mutua anaamini kuwa Waziri Mkuu huyo wa zamani atazungumzia jambo hili "wakati ukifika".

Ni kutokana na wasiwasi huo na tahadhari ya kisiasa kwamba tathmini ya Ichung'wa kumhusu Odinga inaweza kuwa ya kweli kwamba ameingiwa na tumbojoto baada ya wafuasi wake kuanza kumuunga mkono Rais Ruto na kuelekeza masilahi yao zaidi kwa serikali mpya badala ya kuweka matumaini na mustakabali wao nyuma ya kiongozi wa kisiasa ambaye – kutokana na hatima yake ama njama mbaya – hukosea kila mara katika juhudi zake za kushinda urais. Na Ruto anaonekana kufahamu ukweli huu, kulingana na kauli alizotoa katika kaunti

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## kurunzi ya kenya

za Siaya, Kisumu na Homa Bay - zote ngome za Odinga wikendi iliyopita.

Wakati wa ziara yake katika eneo hilo, Rais aliwasihi wakazi wa kaunti hizo tatu waunge mkono serikali yake, akiwakumbusha kuwa "hakuna serikali nyingine mnayongojea."

Ichung'wa anashikilia kuwa Odinga amegundua wananchi, wakiwemo wafuasi wake, wamerudi kwa shughuli zao na "kukubali matokeo ya uchaguzi" na kwamba sasa anajaribu kurudisha nchi katika harakati za uchaguzi ili kudumisha umaarufu wake katika ngome zake za kisiasa.

Lakini Mutua anasema uchaguzi ni mchakato mrefu, mgumu na mchungu ambao hauwezi kumalizika na kutangazwa kwa matokeo ya mwisho wala uamuzi wa Mahakama ya Upeo.

Akidai uchaguzi wa urais ulikumbwa na udanganyifu na utata mwingi, Mutua anadokeza kuwa Raila anatarajiwa kueleza wafuasi wake na Wakenya kwa jumla kilichotokea katika uchaguzi huo: "Watu wataamua watakachofanya na habari hizo. Ni juu yao kuchukua hatua zozote wanazofikiri ni muhimu kurudisha nchi yao.""Sidhani Azimio wataketi tu na kutofanya chochote kuhusu shughuli ambayo waliwekeza sana nguvu zao, jasho, muda na pesa, lakini ikapuuzwa na mahakama kuwa 'hewa moto'. Mheshimiwa Raila atazungumzia hili hivi karibuni, kama alivyoahidi. Na atakapofanya hivyo, itakuwa kauli thabiti ambayo itathibitishwa kwa data na ukweli usiopingika," anasema Mutua.

Akisema kila mtu ana msimamo wake kuhusu uchaguzi wa Agosti na kutoa "madai ya kila aina" kuhusu kilichotokea, yakiwemo madai ya Rais Ruto kwamba watu fulani walitaka kumteka nyara na kumuua Chebukati, Katibu Mkuu wa ODM, Edwin Sifuna, anasisitiza kuwa bosi wake pia ana haki ya kutoa maoni yake.

Bw Sifuna, ambaye ni Seneta wa Kaunti ya Nairobi, anasema mrengo wa Azimio una maelezo yake kuhusu uchaguzi huo, ambayo ni tofauti na yaliyotolewa na kiongozi wa UDA.

Kutokana na simulizi za kila aina kuhusu maisha ya Chebukati na wajibu wa timu yake katika kuendesha chaguzi, Sifuna anachukulia demokrasia ya Kenya kuwa iliyo "hatarini kubwa".

Katika hali kama hiyo, anasema kuwa Odinga – kama mmoja wa wagombeaji wakuu katika uchaguzi wa urais – ana wajibu wa kuelezea ukweli anaofahamu. Duru zilizo karibu na Odinga zinasema "kuelezea ukweli wa mambo kuhusu uchaguzi wa Agosti" ni mmoja wa mipango yake mikuu mwaka huu. Odinga anachukulia hii kuwa habari muhimu inayofaa kutolewa kwa Wakenya,

kando na ukweli kuwa itamuondolea lawama kama kiongozi ambaye hushindwa katika uchaguzi kila wakati. Washirika wake pia wanatumai ufichuzi huo

hatimaye utaelezea historia yake kuhusu msururu wa "kushindwa katika uchaguzi".

Washirika wakuu wa Odinga katika Azimio, viongozi wa Narc-Kenya na Wiper, Martha Karua na Kalonzo Musyoka, pia wanaamini walishindwa katika uchaguzi huo katika hali isiyoeleweka, kwa hivyo wanaunga mkono wazo la kutoa ripoti ya ukaguzi inayoonyesha matokeo kinyume.

Bw Musyoka, kwa mfano, anasema Raila - ambaye alishirikiana naye - hakushindwa katika chaguzi kuu za 2013, 2017 na 2022. Makamu wa Rais huyo wa zamani anatoa wito wa kukomeshwa kwa "mtindo huu uchaguzi kuibwa" na anapendekeza mageuzi katika uchaguzi, ikiwemo kurudishwa kwa uwasilishaji matokeo kwa mikono.

Karua, ambaye alikuwa mgombea mwenza wa Odinga, tayari alishawasilisha kesi katika Mahakama ya Haki Afrika Mashariki kupinga uamuzi wa Mahakama ya Upeo ya Kenya. Waziri huyo wa zamani wa Sheria na

Masuala ya Kikatiba anataka mahakama hiyo ya kanda iamuru mamlaka za Kenya kufanya "uchunguzi wazi, huru, na wa kitaalamu kuhusu ukiukaji wote wa haki" unaodaiwa kufanywa na IEBC na Mahakama ya Upeo ya Kenya.



Muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya unakabiliwa n kibarua kigumu cha kushughulikia maslahi ya washirika wake wa kisiasa, hasa kiongozi wa Wiper Kalonzo Musyoka, ambaye ametangaza nia ya kugombea urais 2027. PICHA | FRANCIS NDERITU

Miaka ya mwanzo baada ya uhuru, uchaguzi wa urais ulikuwa desturi tu, ukiwa na matokeo yaliyopangwa awali. Hasa, Mzee Jomo Kenyatta "alichaguliwa" bila kupingwa miaka yote aliyokuwa rais, sawa tu na ilivyokuwa kwa mrithi wake, Daniel arap Moi, miaka ya 1978, 1983 na 1988.

Uchaguzi ulioonekana kuwa na ushindani ulikuja tu 1992 baada ya kuanzishwa tena kwa siasa za vyama vingi. Katika miaka iliyofuata, hata hivyo, chaguzi zilikuwa na udanganyifu mwingi kwani Serikali ilitumia mamlaka yake. Lakini hali iliharibika mnamo 2007 kufuatia uchaguzi uliokumbwa na udanganyifu, matokeo yake kupingwa na kusababisha ghasia ambapo watu 1,000 walipoteza maisha yao.

Katika kutathmini uwazi wa chaguzi zilizopita, wanasiasa kwa kiasi kikubwa huegemea upande mmoja kwenye tathmini zao na madai kuhusu wizi wa kura.

Musyoka, kwa mfano, hataji uchaguzi wa 2007 miongoni zilizokuwa na wizi wa kura, ilhali huu ndio mwaka ambao wizi ulikuwa wazi.

Mwenyekiti wa iliyokuwa Tume ya Uchaguzi Kenya, Samuel Kivuitu, alikiri

hadharani kuwa hakujua ni nani aliyeshinda uchaguzi wa urais.

Ajabu ni kuwa, Musyoka, ambaye aliwania urais kwa tikiti ya ODM-Kenya, alikuwa katika mrengo sawa wa kisiasa na Karua, ambaye aliongoza harakati za

kumpigia debe Mwai Kibaki kwa tikiti ya Party of National Unity (PNU). Kwa upande mwingine, Ruto, alikuwa mwanachama mkuu wa chama cha Odinga cha ODM na alilalamika vikali kuhusu "wizi" wa kura za kiongozi wa chama chake. Rais alinyamaza kuhusu madai ya kura za Odinga "zilizoibwa" 2007 mara tu alipoungana na mtangulizi wake, Uhuru Kenyatta, mnamo 2013.

Kando ya hayo, huku Musyoka, Karua na washirika wengine wakuu wa Odinga,

wakiwemo manaibu wake Wycliffe Oparanya na Hassan Ali Joho, wakilenga kumrithi kisiasa, mwelekeo wa kiongozi huyo wa ODM ni tofauti.

"Hajali sana kuhusu siasa za urithi katika ODM na Azimio anashughulika zaidi kuunda kikosi chenye nguvu dhidi ya Rais na kumfuatilia kwa karibu kuhakikisha mafanikio ya kidemokrasia yaliyofikiwa baada ya miaka mingi hayatavurugwa akitazama," afisa wa kitaifa wa chama aliyeomba asitajwe jina akaambia 'Darubini ya Wiki.'

Isipokuwa 1997, alipogombea Urais kwa tiketi ya National Development Party of Kenya (NDP) uchaguzi aliotaja kuwa jaribio, Odinga amekuwa akiendesha kampeni kali katika chaguzi zilizofuata, huku akishindwa kwa kura chache au kwa njia yenye utata. Ni hali hiyo ya "kukosa ushindi kwa tundu la sindano" ambayo inawapa wafuasi wake matumaini ya kushindi uchaguzi unaofuata. Hali hiyo imekuwepo kwa miaka mingi, na huku motisha wa kisiasa miongoni mwa wafusi wake ukiwa chini zaidi, kibarua kilicho mbele ya Raila ni kikubwa sana.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

Nation Media Group "ePaper Copy"

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# Hofu huku joto baharini likifika kiwango kipya



Bahari za dunia, ambazo zimefyonza jingi la joto linalosababishwa na binadamu kuchafua mazingira kwa hewa ya kaboni, ziliendelea kupata kiwango cha juu zaidi cha joto mwaka uliopita, kulingana na utafiti mpya.

Mabadiliko ya hali ya hewa yameongeza kiwango cha joto duniani kote, kusababisha kuyumba kwa anga na kuzidisha hali mbaya ya hewa kama vile dhoruba.

Bahari hufyonza karibu asilimia 90 ya joto la ziada kutokana na gesi chafuzi, na kukinga ardhi lakini kusababisha mawimbi ya joto jingi na ya muda mrefu baharini ambayo tayari yana athari mbaya kwa maisha ya chini ya maji. Utafiti huo, uliofanywa na watafiti nchini China, Amerika, Italia na New Zealand, ulisema kuwa 2022 ulikuwa "mwaka wenye kiwango cha juu zaidi cha joto kuwahi kurekodiwa katika bahari za dunia".

Kiwango cha joto katika bahari kilizidi vya mwaka uliotangulia kwa kiasi kikubwa ambacho ni sawa na mara 100 ya uzalishaji wa umeme ulimwengu mzima mnamo 2021, kulingana na waandishi.

"Bahari zinafyonza kiasi kikubwa cha joto kutoka kwa kaboni inayotolewa na binadamu," akasema mwandishi-mwenza Michael Mann, ambaye ni profesa katika Chuo Kikuu cha Pennsylvania.

"Hadi tutakapomaliza kabisa utoaji wa gesi chafuzi, tutaendelea kuvunja rekodi za kiwango cha joto la bahari, kama tulivyofanya mwaka huu," akasema.

Rekodi za tangu miaka ya 1950 zinaonyesha kuwa kupanda kwa joto baharini kumekuwa kukitokea mara kwa mara tangu 1985.

Wanasayansi wameonya kuwa kupanda kwa joto kumeleta mabadiliko makubwa kwa utulivu wa bahari haraka kuliko ilivyofikiriwa awali.

*-Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# MFUMO MPYA ANGANI



Kuweka mtu katika Mwezi kumefanywa awali lakini hatua inayofuata, kuelekea Mars, ni ngumu zaidi.

• LONDON

Kuna mfumo mpya unaojitokeza angani - ushindani kati ya Amerika na China. Lakini kutokana na hamu ya kutalii anga, hata mataifa haya makubwa hayataweza kufanya hivyo peke yake.

Malengo yenye changamoto kubwa ya kiufundi na ya gharama kubwa yamepigiwa debe, kwa mfano lengo la watu kuishi na kufanya kazi kwenye ulimwengu mwingine, labda ndani ya miaka kumi – lakini je, yatafaulu kweli katika katika ulimwengu uliogawanyika ambapo nia njema ya kimataifa ni haba?

Hatua ya Nasa kurudi kwa Mwezi imeanza na mpango wake wa Artemis. Safari ya kwanza kati ya tatu imezinduliwa kwa ufanisi. Safari hii ya ndege isiyo na rubani ilibaini kuwa roketi na teknolojia zilifaulu. Safari ya pili itawapeleka wanadamu mbali zaidi angani kuliko walivyowahi kwenda awali, huku uzinduzi wa tatu ukiweka wanaanga kwenye Mwezi kwa wiki moja, ambapo watafanya majaribio. Lengo la muda mrefu ni kutumia Mwezi kama sehemu ya kuruka ili kufika kwa Sayari Mars.

Lakini mpango huo unakadiriwa kugharimu Sh1.15 trilioni, kiwango cha juu sana kwa mlipa kodi nchini Amerika, ambaye tayari anahisi kubanwa kiuchumi.

Kwenye ripoti yake kwa Bunge la Congress mwaka jana, afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Amerika ilionya kuhusu "ratiba ya maendeleo isiyo ya kweli" na uwezekano wa gharama kubwa, na kuongeza kuwa Nasa ilihitaji kufanya makadirio ya gharama "ya kuaminika zaidi na wazi".

Ingawa Nasa itapata ufadhili mdogo kuliko ilivyoomba 2023, Congress, kwa sasa, bado inaunga mkono shughuli zake za utalii wa anga za juu. China imefanikisha kituo chake cha kufanya kazi kikamilifu, Tiangong, katika obiti kwa wakati. Mpango wa anga za juu wa China umezindua uchunguzi wa Mwezi na Mars. Inapanga kuanzisha kituo cha utafiti kisicho na rubani juu ya Mwezi ifikapo 2025 kisha kufikisha wanaanga katika ardhi ya Mwezi ifikapo 2030.

Kumweka mwanaanga katika ardhi ya Mwezi kumefanywa awali lakini hatua inayofuata, kuelekea Mars, ni ngumu zaidi. Sayari hiyo iko mbali mara 250 zaidi ya Mwezi na hakuna chombo chochote cha anga ya juu kinachoweza kutuma wanadamu kwenye sayari hiyo.

Hata kama wanasayansi wanaweza kutafuta njia salama ya kurusha roketi mafuta mengi na kutua kwenye sayari hiyo yenye angahewa nyembamba namna hiyo, kuna changamoto zaidi ya kuwarudisha wanaanga hao nyumbani salama baada ya kukaa angani kwa miezi kadhaa.

Kihistoria, mataifa makubwa yamepigania udhibiti wa anga. Amerika na Urusi zilizozania kuidhibiti miaka ya 1950 na 1960. Warusi waliweka mtu wa kwanza kwenye obiti. Waamerika walituma mtu na kupanda bendera yao juu ya Mwezi miaka michache baadaye.

Katika miaka ya 1970 enzi ya ushirikiano ilibuniwa na kufikia kilele cha ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Anga (ISS), ambacho kilianza mwaka wa 1998. Pamoja na mataifa mengine 13 washirika, mataifa hayo mawili yenye nguvu zaidi yalijenga kituo kinachoaminika kuwa kikubwa zaidi angani. Hakimilikiwi na taifa lolote, na kila nchi hutegemea nyingine kukiendesha.

Kilikuwa ishara ya kile ambacho binadamu anaweza kufikia kama mataifa yangeweka kando tofauti zake na kufanya kazi pamoja. Lakini ukweli ulikuwa tofauti kwa kiasi fulani. Amerika iilizuia China kuwa mshirika katika ISS, hivyo Wachina wakaenda kivyao.

*-Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya afrika

■ SIMU AMBAZO HAZIKUWA ZINATUMIKA ZILISIKIKA TENA DESEMBA MWAKA JANA

# 'SHUKURU MUNGU UKO HAI'




Abiria wanaowasili kutoka Tigray wakipokewa na jamaa wao katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Bole jijini Addis Ababa Desemba 28, 2022. Shirika la Kitaifa la Ndege Ethiopia lilianza tena safari katika linalokumbwa na vita la Tigray baada ya kufungwa kwa miezi 18.

## Kufuatia kusitishwa kwa vita, simu zilianza kulia tena, wakazi wa Tigray wakifurahi kuwasiliana tena na wapendwa wao walioathiriwa katika mojawapo la mapigano mabaya zaidi duniani

● NAIROBI

Beniam Yetbarek hakujua binamu yake alikuwa hai simu ilipolia Mkesha wa Krismasi, na sauti ambayo hakuwa amesikia kwa miaka miwili ikasikika kutoka Tigray.

Simu kwa familia katika eneo hilo la Ethiopia lililokumbwa na mapigano hazikuwa zikiingia tangu Novemba 2020, huduma za simu na intaneti zilipokatizwa baada ya vita kuanza. Tigray ilitengwa na ulimwengu.

Lakini baada ya kusitishwa kwa vita, simu zilianza kulia tena, na kuleta furaha, lakini pia majonzi na hasira, huku wakazi wa Tigray kama Beniam wakiungana tena na wapendwa wao walioathirika katika mojawapo la mapigano mabaya zaidi duniani.

"Tamko langu la kwanza lilikujwa - shukuru Mungu uko hai. Sijui alivyonusurika miaka hii miwili iliyopita, lakini nafurahi yuko hai," akasema mpiga picha huyo mwenye umri wa miaka 30 kuhusu mazungumzo ya simu na binamu yake anayeishi mjini Axum Desemba 24.

Lakini furaha ilikuwa ya muda mfupi. Familia ya Beniam tayari ilikuwa imempoteza jamaa wao katika vita hivyo na ilikuwa na wasiwasi zaidi binamu huyo alipozungumza kuhusu woga na njaa mjini Axum, wanajeshi wa Eritrea barabarani na mjomba wake mgonjwa asiyeweza kupata dawa ya kisukari.

Huku wamezunguka simu hiyo, walijua pia kuwa shangazi yao alikufa katika miezi ambayo hapakuwa na mawasiliano ilhali binamu hakujulikana aliko na ilidhaniwa alikufa.

"Habari hizo zilimaliza hewa chumbani," Beniam akaambia AFP kutoka Seatle. "Shanga-

...Endelea Uk 26

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Machozi huku simu zikisikika tena Tigray

Kutoka Uk 25

zi yangu alianza kulia. Binamu wangu wawili walibaki kimya. . .Tulikuwa tukijaribu kupata habari zote, lakini alipokata simu, sote tukaanza kuomba kimya kimya."

Huduma za simu zilirudishwa katika sehemu kadhaa za Tigray mapema 2021 kabla ya kukatizwa tena Juni mwaka huo.

Simu zilianza kusikika tena Desemba mwaka jana, mwezi mmoja baada ya kusitishwa kwa mapigano katika mzozo ambao Mataifa ya Magharibi yanakadiria ulisababisha kuuawa kwa kati ya watu 100,000 na nusu milioni.

Mkataba wa amani ulipelekea kufunguliwa upya kwa Tigray, eneo la watu milioni sita, na kuondolewa kwa amri ya kutosafiri iliyowekwa na serikali ya Ethiopia.

Katika mji wa Mekele, umati ulifurika katika maduka ya simu siku baada ya siku kurudisha nambari zao za zamani za simu, akasema mwanamke mwenye umri wa miaka 29, aliyefika mjini humo baada ya safari za ndege kurudi Desemba 28. "Mama yangu alilia aliposikia sauti yangu baada ya miezi hii yote. Nililia pia," akasema mwanamume mwenye umri wa miaka 42 jijini Addis Ababa, aliyeongea na AFP na kuomba asitambuliwe kutokana na sababu za kiusalama.

Wengine, hata hivyo, wamepokea habari za kuvunja moyo. "Walimuua nje ya nyumba yake," akasema Maharit Gebreyesus kuhusu mjamba wake, mmoja kati ya jamaa zake saba aliofahamishwa waliuawa na wanajeshi wa Eritrea karibu na Adwa mwishoni mwa Oktoba.

Shangazi yake alikuwa salama Adwa, alikokimbilia usalama baada ya kijiji chake kuporwa na kuchomwa moto. Simulizi ya msiba ilitoka kwa Mkuu wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) Tedros Adhanom Ghebreyesus, akisema mjamba wake pia aliuawa na wanajeshi wa Eritrea.

Wanahabari wa kigeni wamezuia kuingia Tigray na AFP haiwezi kuthibitisha yenyewe habari hizi. Lakini pande zote katika mzozo wa Tigray zimelaumiwa na waangalizi huru wa mapigano, na kutuhumiwa kwa mauaji ya kikabila na kuwakosesha watu chakula kimakusudi.

Beniam alisema hali ya kutojua hatima ya familia yake mjini Axum - ambako mamia ya raia waliuawa Novemba 2020 – inamsumbua akili. "Singemtakia adui yangu mkubwa matukio ya miaka miwili iliyopita," akasema. "Uzito wa taharuki hiyo unaweza kukuua."

Mwanamke mwenye umri wa miaka 25 aliambia AFP "alishindwa kuongea" dada yake alipompigia simu ghafla kutoka Shire, mji ulioshambuliwa Oktoba, kusema familia yake ilikuwa salama. Lakini pia alikasirika kwa kuwekwa gizani kwa muda mrefu. "Siamini kuwa katika karne hii, nililazimika kuota . . . ili kuzungumza na familia (kujua) iwapo walikuwa hai au la," akasema.

Zaidi ya miezi miwili baada ya pande mbili pinzani kutia saini mkataba wa amani, huduma bado ni haba katika miji mikubwa, huku simu zikikatika baada ya dakika chache, au kukosa kuingia kabisa. "Kusema kweli, ilibidi tupige simu zaidi ya mara 100 ili kuingia," akasema mwanamke mwenye umri wa miaka 40 aliyeongea na wazazi wake kwa mara ya kwanza Januari 3, baada ya miezi 18.



Mwanamume katika vitongoji vya mji wa Mai Kadra, Ethiopia. Simu kwa familia katika eneo la vita la Tigray hazikuwa zikienda tangu Novemba 2020, ambapo huduma za simu na intaneti zilikatwa.

Kampuni ya umeme ya serikali ilisema Jumanne stima itarudishwa kikamilifu Tigray ndani ya wiki mbili. Msemaji wa Waziri Mkuu Abiy Ahmed aliambia AFP miundomsingi muhimu imekarabatiwa na huduma za simu kurudi katika miji 51 eneo la Tigray. Hata hivyo, hakusema ni lini mawasiliano kamili yatarudi.

Tulipotaka maelezo kutoka kwa Ethio Telecom, shirika la mawasiliano la serikali, simu zetu hazikujibiwa. Wakati huo huo, Meharit hawezi kumfikia baba yake mwenye umri wa miaka 65 au dada zake sita mjini Negash, kusini mwa Tigray, na hana la kufanya ila tu kuomba wapokee simu. "Sijui kama yuko hai au la," akaambia AFP.

Jeshi la Ethiopia lilitangaza kuondolewa kwa kikosi cha wanajeshi wa mataifa ya kanda hii kutoka mji muhimu wa Tigray chini ya mkataba wa amani kukomesha vita hivyo vya miaka miwili huku mawaziri wa mataifa ya Ulaya waliozuru nchi hiyo wakisema hakuwezi kuwa na maridhiano bila haki.

Mawaziri wa Mashauri ya Kigeni wa Ujerumani na Ufaransa walizuru Ethiopia siku moja baada ya waasi wa Tigray kutangaza kusalimisha silaha - hatua mojawapo muhimu ya mkataba wa Novemba 2 wa kukomesha vita katika nchi hiyo ya pili kwa idadi kubwa ya watu baranifrika.

Mnamo Alhamisi jeshi la Ethiopia lilisema vikosi maalumu vya Amhara - jeshi la kikanda liliounga mkono serikali ya Ethiopia katika vita hivyo - viliondoka kutoka mji wa Shire, hatua iliyotimiza sehemu nyingine muhimu ya mkataba huo wa Amani.

Mapigano kaskazini mwa Ethiopia kati ya serikali ya majimbo na waasi wa Tigray People's Liberation Front (TPLF) yameangamiza maisha ya wengi. Waziri wa Mashauri ya Kigeni wa Ufaransa Catherine Colonna alisema anaunga mkono "hatua nzuri ambazo zimefikiwa" katika mkataba wa amani. "Uhasama umekoma, msaada umeweza kufika maeneo ambako haukuwa umefikia. . . waasi wameanza kusalimisha silaha," akaambia wanahabri akiandamana na mwenzake wa Ujerumani, Annalena Baerbock.

Lakini mawaziri hao walihimiza kuanzishwa kwa mpango wa kuwaadhibu waliotekeleza ukatili wakati wa mapigano hayo. Sisi, Wajerumani na Wafaransa, tunajua maridhiano hayafanyiki haraka. Lakini bila matumaini ya haki kwa waathiriwa wa uhalifu, maridhiano na amani ya kudumu hayawezi kufikiwa," akasema Baerbock.

"Suala la uwajibikaji ni muhimu kwetu kwa kuzingatia mustakabali na amani Ethiopia, lakini pia katika kuimarisha sheria ya kimataifa," akasema baada ya mazungumzo na Waziri Mkuu Abiy Ahmed. Naibu Waziri Mkuu wa Ethiopia ambaye pia ni Waziri wa Mashauri ya Kigeni Demeke Mekonnen aliambia wanahabari serikali yake itahakikisha waliotenda uhalifu wameadhibiwa.


*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## kurunzi ya dunia

■ MASANDUKU, BIDHAA ZA WATOTO NA CHAKULA ZILITAPAKAA

# MAUAJI KATIKA KITUO CHA TRENI




Kituo cha treni, kikionekana kupitia kwa kioo kilichovunjwa cha dirisha la treni kufuatia shambulio la roketi mjini Kramatorsk, mashariki mwa Ukraine, mnamo Aprili 8, 2022, raia walipokuwa wakitoroka eneo la Donbas, wakihofia kuvamiwa na wanajeshi wa Urusi. Watu 61 waliuawa katika shambulio hilo wakiwemo watoto saba.

**Licha ya kimya kingi kuhusu shambulizi la kikatili mnamo Aprili mwaka jana - mojawapo la mabaya zaidi katika vita hivyo - limeacha alama isiyofutika kwa manusura na waliolishuhudia**

• KRAMATORSK

Shambulizi la kombora katika kituo cha reli cha Kramatorsk Aprili mwaka jana, ambalo liliua watu wengi, halizungumziwi katika jiji hilo karibu na maeneo ya msitari wa mbele ya vita mashariki mwa Ukraine.

Licha ya kimya kingi kuhusu shambulizi hilo la kikatili- mojawapo la mabaya zaidi katika vita hivyo - limeacha alama isiyofutika kwa manusura na walioshuhudia.

Karibu mwaka mmoja baadaye, kuna ishara chache katika jengo dogo la matofali rangi nyekundu za matukio yaliyotikisa jamii ya eneo hilo ambayo haijawa na muda wa kupona na kufikiri huku vita vikiendelea.

Gari moshi lilioundwa miaka ya 1940 linasimama mbele ya kituo hicho, katika eneo ambalo sehemu nyingine ya jiji hilo la viwanda ilijengwa kuanzia karne ya 19.

Asubuhi ya Aprili 8, raia wanaokadiriwa kuwa 4000 walikusanyika kupanda magari ya kuwahamisha wanajeshi wa Urusi walipokaribia. Saa nne na nusu asubuhi, kituo hicho kilishambuliwa kwa kombora aina ya Tochka-U, ambalo kulingana na wataalamu, lilikuwa na vilipuzi vingi. Watu 61 waliuawa na zaidi ya 160 wakajeruhiwa, ofisi ya Meya ilisema.

Shambulio hilo ni mojawapo la madai kadhaa ya uhalifu wa kivita dhidi ya Urusi tangu kuanza kwa vita hivyo, pamoja na kuuawa kwa raia eneo la Bucha karibu na mji wa Kyiv, na vita vya Mariupol. Maeneo hayo, sawa na Kramatorsk, yamepitia mateso makubwa kutokana na ukatili wa vita hivyo.

Upande wa kulia wa jukwaa kuu la kituo cha Kramatorsk ambako wengi wa waathiriwa walifariki, bado kuna dalili za uharibifu kutokana na mlipuko huo.

Shada dogo la maua na vifaa vya watoto vimeanguka karibu na vyuma vya kituo ukumbusho wa watoto saba walioathiriwa. Jiwe kubwa limeandikwa: "Kutaku-

Endelea Uk 28

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Uchungu sana: Shambulio katika kituo cha treni

Kutoka Uk 27

wa na ukumbusho wa waathiriwa wa Aprili 8, 2022 hapa." Walipofika katika kituo hicho punde tu baada ya shambulio hilo siku hiyo, wanahabari wa AFP waliona mili 30 katika mifuko, na barabara zilizojaa damu.

Masanduku, bidhaa za watoto na vyakula vilitapakaa katika eneo hili. Hadi leo, wenye maduka na madereva wa teksi karibu na kituo hicho hutoa maelezo ya jumla kuhusu kilichotokea, bila kutaja shambulio hilo.

"Sio vizuri kukumbuka," akasema Alexander, muuzaji mboga katika kituo hicho kwa miaka 20. Kituo cha Kramatorsk kilifunguliwa upya Oktoba, miezi sita baada ya shambulio hilo, na kudumisha msimamizi wake, mwanamke mdogo mwenye nguvu aliye na nywele fupi ya kahawia, ambaye alikuwa kazini asubuhi hiyo. Amekataa kuzungumza na maripota.

"Mnataka niseme nini? Mili iliyokatwakatwa, damu, vilio. Ilitisha, ilitisha!" akawafokea wanahabari wa AFP mnamo Julai. Kabla na tangu wakati huo, amekataa mahojiano yoyote.

Mykola Byba, kamanda wa zima moto, bado huepuka kutembea karibu na kituo hicho miezi kadhaa baadaye. "Ni uchungu sana," akasema Byba, akizungumza na AFP katika kituo cha zima moto cha eno hilo.

"Asubuhi hiyo, nilikuwa nimefika mapema nikiwa na wenzangu wawili kupanga jinsi ya kuhamisha watu. Kisha nikarudi katika kituo cha zima moto," akasema.

Wazima moto, polisi, waliojitolea na wafanyakazi wa jiji walikuwa wakisaidia raia kutorokea magharibi, kufuatia wito wa serikali ya Ukraine kwamba wato waondoke.

Ofisi ya meya ilisema watu wapatao 80,000 waliondolewa kutoka Kramatorsk kati ya kuanza kwa uvamazi wa Urusi Februari 24, 2022 na siku ya shambulio hilo. "Nakumbuka mlipuko wa kwanza. Mkubwa sana. Kisha wa pili, ulikuwa mdogo," akasema Byba. Yeye na wenzake walikimbia katika kituo hicho.

"Tulipofika, tuligundua mara moja kiwango cha mkasa huo. Kulikuwa na hali za kutisha. Lakini ninachokumbuka sana ni harufu kali ya damu, kali, kali sana." Wazima moto walijaribu kuzima magari yaliyokuwa yakichomeka na kutibu majeruhi. "Walikuwa wakifa mikononi mwetu," akasema Byba.

Anton Malinsky, mfanyakazi wa baraza, alisema umati uliokuwa katika kituo hicho ulitoka sehemu zote za eneo hilo. "Nilikuwa mita chache kutoka kituoni. Mlipuko ulikuwa mkubwa kiasi kwamba baadhi ya watu walianza kutokwa na damu katika mapua yao," akasema. Kisha alianguka na kukanyagwa na umati uliokuwa umeshtuka. "Nilikuwa afisa wa polisi na ninajua jinsi ya kujizuia kuumia. Sikufikira hilo," akasema.

Mkahawa karibu na kituo hicho uliopambwa na picha za Eiffel Tower ulifunguliwa wiki chache zilizopita. Hapo, mhudumu wa kujitolea kusaidia binadamu Natalya Slobodyan alisema maisha yanarudi pole pole katika jiji hilo kufuatia ukombozi wa Ukraine. "Watu wanarudi. Maisha yanarudi. Hali inaimarika," akasema mama huyo wa watoto watatu mwenye umri wa miaka 36.



Wanasesere waliowekwa karibu na kituo cha treni mjini Kramatorsk, eneo la Donetsk mnamo Januari 16 amnako watu 61 waliuawa na kombora katika uvamizi wa Urusi nchini Ukraine Aprili 8, 2022. Raia wapatao 4,000 walikuwa wakitoroka wanajeshi wa Urusi.

Baada ya uvamizi wa Urusi kuanza, Slobodyan alijianza kazi ya kujitolea kuepuka msongo wa mawazo. Mnamo Aprili 8, alitakiwa kuchukua dawa katika kituo hicho. "Wakati mwingine maisha hukuonyesha dalili. Watoto walikuwa wakilia na gari ilikataa kuwaka. . .mlipuko ulipotokea - sauti ambayo itadumu katika masikio yangu milele - bado nilikuwa nyumbani," akasema.

Bado aliendа katika kituo hicho baada ya mlipuko. "Kitu cha kwanza kuona ni mtoto aliyekufa. Kisha machafuko kila mahali," akasema. Mmoja wa marafiki zake wakubwa aliuawa siku hiyo, akakumbuka, akitaja kufunguliwa kwa kituo hicho kuwa "maajabu".

Baada ya kituo hicho kulipuliwa, Ukraine na watu mashuhuri kimataifa waliapa kuwaandama waliotekeleza "uhalifu wa kivita". Ofisi ya mkuu wa mashtaka wa Ukraine, inayoongoza uchunguzi huo, ilikataa kuzungumza na AFP. Mnamo Oktoba 2022, wachunguzi wa kidijitali kutoka kituo cha Centre for Information Resilience (CIR), shirika lisilo la kiserikali, walisema ushahidi wa shirika hilo ulionyesha "Urusi inaweza kuwa ilihusika".

"Tulianza uchunguzi wetu siku ya mkasa," akasema Pierre Vaux, mmoja wa waandishi. Wachunguzi walisaidiwa na video nyingi na jumbe za mitandao ya kijamii zilizochapishwa mkesha wa na siku ya shambulio. Miongoni mwa jumbe hizo lilikuwa onyo kutoka kwa waasi wanaounga mkono Urusi mnamo Aprili 7 dhidi ya kuhamisha watu kwa treni.

Urusi imekanusha kuhusika, ikidai haina kombora aina ya Tochka-U lililotumiwa, akitaja madai hayo kuwa "uchokozi" wa Ukraine.

Wanahabari wa AFP waliona maneno ya Kirusi "Kwa watoto" - tamko linalotumiwa na waasi wanaounga mkono Urusi – yameandikwa kwenye kipande cha kombora.

Hakuna orodha rasmi ya waathiriwa wote imewahi kuchapishwa na nyingi za familia zilizoathiriwa zimeondoka eneo hilo au zimekataa kuzungumza.

Miongoni mwa waliokufa ni "mwalimu, mfanyakazi wa maktaba, vijana na watoto wakiwa na mama zao," akasema Oleksiy Ladyka, mwanahabari wa gazeti la Kramatorsk Post. Ladyka ametambua wengi wa waathiriwa na amefungua kumbukumbu mtandaoni.

"Ilikuwa kazi ngumu sana," Ladyka akaambia AFP. "Maafisa wa eneo hilo hawakuwa na majina yao. Jeshi haikutuambia chochote. Tuliyatafuta sisi wenyewe, kupitia mitandao ya kijamii, kupitia duru zetu.

"Ilikuwa ngumu zaidi kwa sababu waathiriwa walitoka sehemu tofauti eneo hili." Kumbukumbu yake ina majina 26, picha na mistari michache kueleza maisha ya kila mmoja.

"Tutashughulikia yaliyopita baada ya vita," akasema Andrei Bessonny, naibu meya wa Kramatorsk. "Nilikuwa hapo Aprili 8. Nilijionea. Siku kadhaa baada ya mlipuko, bado tulikuwa tukipata vipande vya binadamu katika sehemu tofauti za kituo hicho.

"Ni mkasa mbaya zaidi ambao jiji hili limewahi kupata kwa kuzingatia idadi ya waathiriwa. Lakini vinaendelea, havijaisha. Viko kila siku. . .Warusi tayari wameharibu nusu ya nchi. Pengine tumezoea, pengine hatujali tena."

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya dunia

■ HUENDA WAANDAMANAJI WA JANUARI 8 WALIMPA NGUVU

# LULA: MTU ASIYETIKISIKA

• BRASILIA

Kwa kuvamia na kupora mali katika majengo ya serikali kupinga kiongozi wa mrengo wa kushoto Luiz Inacio Lula da Silva, huenda waandamanaji wa Januari 8, Brazil wamempa nguvu, ingawa kwa muda, wachanganuzi wanasema.

Wengi, wakiwemo wafuasi wa rais wa zamani aliyeshindwa, Jair Bolsonaro, aliyeegemea mrengo wa kulia, walishangazwa na uharibifu uliofanywa katika majengo ya kitaifa na vito vya kale. Ghafla baada ya uvamizi wa afisi ya rais, Bunge na Mahakama ya Juu, Lula aliwaita pamoja viongozi wa asasi hizo tatu - wengi wao wanaoegemea mrengo wa kulia kisiasa - kulaani matukio hayo.

Wakionyesha umoja, walibaini hadharani kwamba demokrasia haitaruhusiwa kuyumba miongo mitatu baada ya kuanguka kwa utawala wa kidekteta wa kijeshi Brazil. "Matukio ya Januari 8 yalikuwa na matokeo yaliyokwenda kinyume na yaliyokusudiwa," akasema Mayra Goulart, Profesa wa sayansi ya siasa katika Chuo Kikuu cha Federal University of Rio de Janeiro. "Bila shaka Lula ataibuka mwenye nguvu zaidi. Mashambulio hayo yameleta hali ya umoja wa kitaifa kulinda demokrasia," akaambia AFP.

Machafuko hayo yalitokea wiki moja kamili baada ya kuapishwa kwa Lula katika hafla ya kufana, lakini bila kuwepo kwa Bolsonaro, aliyeondoka siku mbili zilizotangulia na kukwepa wajibu wa kumpokeza ala za mamlaka ya urais.


Maelfu ya watu waliingia katika taasisi za serikali, wakavunja madirisha na fanicha, wakaharibu vinyago huku wakiacha jumbe zinazohimiza mapinduzi ya kijeshi. Jeshi halikutikia wito huo. Watu zaidi ya 2,000 waliodaiwa kuwa waandamanaji walizuiliwa na maafisa wanasaka wanaoshukiwa kupanga na kufadhili maasi hayo yaliyotikisa Brazil na dunia.

Uchunguzi umeanzishwa kuhusu uwezekano wa kuhusika kwa Bolsonaro, ambaye waziri wake wa haki alikamatwa Jumamosi kwa tuhuma za kushirikiana na wavamizi hao. Mataifa ya nje yaliungana kulaani vitendo hivyo.

Amerika, Urusi, China, Umoja wa Ulaya, Ufaransa na mataifa ya Latin Amerika yalisema yanaunga mkono rais mpya wa Brazil - taifa ambalo lilitengwa kimataifa chini ya utawala wa Bolsonaro. "Shutuma za kimataifa zitaimarisha nafasi ya Lula, atakayeonekana kuwa kiongozi muhimu atakayechangia sana katika majukwaa ya kimataifa," akasema Goulart.

Leandro Gabiati wa kampuni ya ushauri ya Dominium, alisema hadhi ya Lula "imeimarishwa" kutokana na namna alivyoshughulikia operesheni ya kunasa wahusika wa machafuko hayo. Kwa upande mwingine hadhi ya Bolsonaro imeharibiwa. Lula "alikabiliwa na upinzani na akafanya vizuri," akasema Gabiari, akitaja hatua ya rais huyo iliyorudisha hali ya kawaida, bila kuonekana kulipiza kisasi.

**Rais anakabiliwa na kazi ngumu katika kuponya nchi inyokabiliwa na migawanyiko kutokana na kampeni kali ya uchaguzi iliyojaa porojo na vitisho**


Rais Lula da Silva

Serikali ya Lula imekuwa thabiti. Watakaopatikana na hatia ya kuhusika katika machafuko watakabiliwa na kifungo cha hadi miaka 30 kwa kosa la "ugaidi". Huku waliopanga maasi hayo wakisakwa, serikali ilitangaza mabadiliko katika polisi na vikosi vya usalama. Ilitangaza kuwa kuwa walinda usalama katika kasri la rais pia watafanyiwa mabadiliko kuwaondoa waaminifu kwa Bolsonaro waliobakia. Lula atalazimika "kuweka vikwazo ili kuzuia marudio ya aina hii ya maandamano," akasema Gabiati.

Na huku akihitajika kushughulikia haraka matatizo kama umaskini na njaa, Lula atalazimika "kutumia nguvu katika uchunguzi…. dhidi ya waliotaka kupindua serikali," akaongeza msomi Goulart. Wakati huo huo, kazi za serikali ziliendelea wiki hii, huku sherehe zikifanywa katika majengo rasmi ya serikali kuapisha mawaziri wapya wa Lula. Hii ni licha ya kuwepo kwa vipande vya glasi na fanicha zilizovunja na waandamanaji.

Lula atakabiliwa na kibarua kigumu cha kujaribu kuponyesha nchi yenye migawanyiko kutokana na kampeni za uchaguzi zilizojaa porojo na vitisho. Mwanasiasa huyo wa mrengo wa kushoto alipata ushindi mwembamba wa kura 60 milioni huku Bolsonaro akipata kura 58 milioni.

Wapinzani wakuu wa Lula - wakichochewa na kauli za kikomunisti na kutokubali matokeo ya uchaguzi - huenda wasivunjike moyo. "Nafikiri kilichofanyika Januari 8, kilikuwa mshtuko mkubwa. Na nafikiri wengi wa watu waliompigia kura Bolsonaro hawakutarajia au kuunga mkono kilichotendeka," akasema Michael Shifter, afisi mkuu katika shirika la Inter-Amerika Dialogue. Hata miongoni mwa waliounga mkono machafuko hayo, wengi walivunjwa moyo na kushindwa kwa wanajeshi kuingilia kati kuwasaidia, mchanganuzi huyo akaambia AFP.

"Nafikiri kile tunaona (vuguvugu la kupinga Lula) ni wapinzani wasio na umoja. Na nchi sasa, ilivyotarajiwa imeungana nyuma na Lula," akasema Shifter. "Lakini nafikiri vuguvugu hili bado lipo na huenda tukashuhudia visa vichache vya misukosuko, maandamano na fujo," akaongeza.

"Sidhani hali hiyo itatoweka,"

**— AFP**

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

TANZIA

■ SAFARI YAKE HADI CHUMBA CHA HABARI ILIANZA KWA AJALI MIAKA 15 ILIYOPITA

# OERI APIGA YAKE MWISHO

● NA ERIC SHIMOLI

Ilikuwa moja ya ajali zilizompeleka mtu katika chumba cha habari. William Oeri alikuwa mwanajeshi, aliyefunzwa kuua na kuharibu. Lakini pia alibeba kamera. Katika utangamano wangu na wanajeshi na polisi, nilijua mtu yeyote katika sekta ya usalama aliyebeba kamera pia alihudumu kama afisa wa upelelezi. Oeri alipewa kazi maalumu katika Kambi ya Kijeshi ya Moi Airbase, Eastleigh, Nairobi.

Vyumba vya habari kote duniani huvutia watu kutoka taaluma tofauti. Kuna walimu, wanafunzi wa zamani wa upadri, wanauchumi, wanasheria na hata maafisa wa zamani wa polisi. Lakini haikuwa kawaida kwa mwanajeshi kujiunga na vyombo vya habari.

Safari ya Oeri hadi chumba cha habari ilikuwa ajali miaka 15 iliyopita. Ndege ya kijeshi ilianguka katika uwanja wa ndege wa Eastleigh asubuhi moja lakini Jeshi la Angani Kenya (KAF) lilikuwa limezuia vikali habari kuhusu tukio hilo. Visa vya aina hiyo vilikuwa vimeongezeka na jeshi liliona aibu kutokana na maswali yaliyoulizwa na vyombo vya habari na umma kuhusu kiwango cha mafunzo ya wafanyakazi wetu katika jeshi na udumishaji wa ndege.

Wanahabari waliofika kuripoti ajali hiyo walifungiwa nje ya Air Base na kulikuwa na habari kidogo huru za kuthibitisha ajali hiyo. Lakini wanahabari wa Daily Nation kwenye tovuti na katika chumba cha habari walifanikiwa kukusanya taarifa na kuweka pamoja ripoti ya kuaminika kuhusu tukio hilo, ambayo ilichapishwa. Pia tulipata picha za ndege iliyoanguka. Ripoti hiyo iliudhi washindani wetu ambao walikosa ripoti hiyo pamoja na pia wakuu wa jeshi wakati huo.

Jeshi liliamuru uchunguzi wa ndani kufanywa ili kujua jinsi habari hizo zilivyotolewa na kwa njia fulani Oeri akaelekezewa kidole cha lawama. Sijawahi kujua jinsi wakuu wa kijeshi walivyofikia uamuzi huo, lakini ulikuwa na gharama kubwa ya kibinafsi kwa Oeri na familia yake changa, ambayo ilikuwa ikiishi katika kambi ya Air Base.

Kama ilivyo kwaida kwa matukio ambapo mtu anashtakiwa na kupatikana na hatia katika jeshi, Oeri alikamatwa upesi, akazuiliwa na hatimaye kuachiliwa bila heshima na kusukumwa nje ya Kambi ya Jeshi. Mkewe, Faith, na watoto, ambao walikuwa wakiishi katika makao ya jeshi, walifukuzwa na hawakuwa na mahali pa kwenda.

Asubuhi iliyofuata, Faith, aliyefadhaika sana, alikuja katika chumba cha habari cha NMG na kufichua kwamba familia ilikuwa imefukuzwa na Oeri kufutwa kazi. Catherine Gicheru, ambaye wakati huo alikuwa mhariri wa habari nami (naibu mhariri wa habari) tulilazimika kubuni mpango wa kuokoa familia hiyo, ambapo kwa usaidizi wa Meneja wa Usimamizi wa Wahariri, David Aduda, Mhariri Mkuu Joseph Odindo na Mkurugenzi Mkuu wa Uhariri Wangethi Mwangi, walimpa kazi kuwa mpiga picha wa mkataba ili kumsaidia kutulia nje ya maisha ya kijeshi.

> Iwe anatazama chini ya lenzi ya bunduki au lenzi ya kamera, William Oeri aliishi maisha marefu na yenye matukio mengi katika jeshi na vyombo vya habari.



William Oeri

Kama kawaida yake, Oeri alifanya kazi zake kwa uchangamfu na nguvu lakini hakusaliti uaminifu wake wa kijeshi. Ilikuwa aibu kwamba jeshi lilimpiga marufuku kuzuru katika kituo chochote chao, au kupanda ndege au magari yao, lakini Oeri alibaki kuwa mwanajeshi mwaminifu hata wakati wake katika chumba cha habari cha Nation Media Group (NMG), alikopanda cheo hadi kuwa Naibu Mhariri wa Picha na baadaye kuhamia gazeti la People Daily.

Mara pekee alipokaribia kufichua maisha yake katika jeshi ni pale alipoambia kundi la marafiki wake jinsi alivyokuwa sehemu kikosi cha operesheni maalumu kumtoa Rais wa zamani wa Somalia, Mohammed Siad Barre kutoka Somalia kumleta Kenya waasi walipokuwa karibu kivamia kasri lake. Wakati mwingine, Oeri alilinda siri nyingi kuhusu wanajeshi na aliwatazama wenzake kama watu wasiojua masuala ya ulinzi. Jambo la kusikitisha ni kuwa NMG ilikosa nafasi ya kumtuma Oeri kuangazia harakati za Jeshi la Kenya (KDF) likikabili kundi la Al Shabaab nchini Somalia kutokana na kupigwa marufuku kwake.

Ni dhihirisho la jinsi mtu huyo alikuwa wa kipekee kwamba, licha ya kupoteza marupurupu yake yote baada ya kutimuliwa kutoka jeshini, Oeri alitumia kazi yake ya uanahabari kujenga himaya ya kibiashara ya ajabu katika maeneo ya Kahawa, Nairobi, Ongata Rongai na Nanyuki. Alikuwa amewekeza katika vyumba, maduka na kilimo, miongoni mwa biashara nyingine, na alikuwa mwepesi kuwatia moyo wafanyakazi wenzake kuhusu kulikokuwa na fursa za kibiashara. Waliofanya kazi naye na kumfahamu walimuita OC (Officer Commanding) Press – maana yake - Afisa Kamanda wa Wanahabari. William Oeri alifariki kwenye ajali katika barabara ya Kenol-Sagana mnamo Januari 15. Buariani OC Press.


***eshimoli@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep








**SMS the word GAZETI to 20567,**
Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE SMS text and FREE Delivery**

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

**Terms & Conditions apply***


SPORT ON!
JAMES WOKABI
BERNARD NDONG
HOSTS
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
SATURDAYS 3PM